Haliuzwi

MEI 25, 2026

/islamicftz

Dhul-Hijja 0 1447

# IMAAN

ISSN 5618 - NO. 585

Huwatoa watu gizani kwa idhini ya Allah

## Mivutano ya hijab mashuleni Kenya yaibua mjadala wa uhuru wa dini



# Hofu ya vita yashindwa kuteteresha Hijja

- Saudi Arabia yaonya Hijja isitumike kinyume na ibada
- Muongozo wa kupanga matumizi ya fedha kwa ajili ya Eid
- Swala ya Eid: Ibada ya furaha, umoja na kumshukuru Allah
- Marekani yaonywa isianzishe vita siku za ibada ya Hijja



## CIFCA: Hifadhi ya jamii kwa misingi ya Kiislamu Tanzania inawezekana

Mikakati ya Serikali kudhibiti upandaji holela bei za bidhaa

## Rais Mwinyi: Sina nia kuongezewa muda wa uongozi, miaka 10 yatosha

## Imaan Media yazindua kadi za wachangiaji





Mwenyekiti wa taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahdi akizungumza katika uzinduzi wa kadi maalum za wachangiaji wa Vyombo vya Habari vya Imaan uliofanyika katika Studio za TV Imaan.

## Dhulma dhidi ya waqfu: Makosa makuu na hatari ya kupotea kwa amana za Allah Tanzania

**HABARI**
**DAR ES SALAAM**

NA MWANDISHI WETU

# Imaan Media yazindua kadi za wachangiaji

MWENYEKITI wa taasisi ya The Islamic Foundation amezindua kadi maalum za wachangiaji wa Vyombo vya Habari vya Imaan.

Uzinduzi huo ulifanyika katika Studio za TV kupitia kipindi maalum kilichorushwa Jumapili Mei 24, kuanzia saa 3:45 usiku na kufuatiliwa na maelfu ya Watanzania.

Sehemu ya fedha kutoka katika kampeni hiyo ya kutunisha mfuko wa kugharamia uendeshaji wa vyombo hivyo itatumika katika upanuzi wa Radio Imaan kwenda kuwa ya kitaifa kutoka sasa ambapo matangazo yake yanafika mikoa 10 pekee.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti Nahdi, zaidi ya shilingi milioni 220 zinahitajika kwa ajili ya zoezi hilo la kufungua vituo 10 vipya vya kurushia matangazo ili kuweza kufikisha matangazo hadi mikoa 20.

Akitaja malengo ya mpango huo, Mwenyekiti Nahdi alisema ni kuongeza ushiriki wa Waislamu katika katika uendeshaji wa vyombo ili kuwafanya kuwa sehemu ya wadau muhimu katika kusukuma gurudumu la uenezi wa da'awah, elimu ya Uislamu sambamba na habari kwa mtazamo wa Kiislamu.

Akifafanua mpango huo, Mwenyekiti alisema wanachama hao watasajiliwa katka makundi ya kadi za thamani tofauti na kutengeneza kanzidata ya wachangiaji watakaulipa michango yao hiyo kila mwezi.

Alisema kujisajili katika mpango huo ni ahadi ya kuchangia kiwango husika kila mwezi lakini alifafanua kuwa hiyo haizuii mpango wa kawaida wa kujitolea usiombatana na mfumo huo wa kadi. "Ukiwa umejisajili katika kiwango mpango wa kadi fulani bado unaweza kuendelea kuchangia katika michango ya kawaida kila unapopata pesa," alisema

Akifafanua makundi hayo ya kadi, Mkurugenzi wa Utawala wa taasisi hiyo, Arafat Badru alitaja kuwa kiwango cha chini cha kadi hizo za uchangiaji kwa mwezi ni Tsh 1,000/= (kadi ya Maroon), ikifuatiwa na Tsh 5,000/= (Blue), 10,000/= (Green).

Viwango vingine vya uchangiaji kwa mwezi ni Tsh 100,000/= (kwa wenye kadi ya Bronze), Tsh 200,000 (Silver), Tsh 300,000/= (Gold) na Tsh 500,000/= (Platinum).

Ukiacha kuwa sadaka kwa watoaji ambayo Mwenyezi Mungu pekee ndiye atawalipa, lakini Badru pia amesema wachangiaji hao watapewa kipaumbele katika matukio ya taasisi ikiwa ni ishara ya kuwashukuru kwa mchango wao.

Wasikilizaji kadhaa walipiga simu kuuliza maswali na kutoa maoni ambapo wengi wao walikuwa wakitoa maombi mikoa yao ipewe kipaumbele katika utanuzi wa huduma za Radio Imaan huku wengine wakitoa ahadi katika usajili wa kadi za viwango walivyochagua.












ذو الحجة

HABARI
DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# CIFCA: Hifadhi ya jamii kwa misingi ya Kiislamu Tanzania inawezekana

Wataalamu wa fedha za Kiislamu wameeleza kuwa Tanzania ina nafasi kubwa ya kuanzisha huduma za hifadhi ya jamii zinazozingatia misingi ya Kiislamu, huku wakisisitiza umuhimu wa kujenga uelewa, kuimarisha mifumo ya kidijitali na kushirikisha wadau mbalimbali ili kufanikisha lengo hilo.




Kauli hiyo ilitolewa katika Mdahalo wa 7 wa Kila Mwezi wa Fedha za Kiislamu ulioandaliwa na Kituo cha Ushauri na Uzingatiaji wa Fedha za Kiislamu (CIFCA) jijini Dar es Salaam, ukiwa na mada isemayo: "Umuhimu wa Kuanzisha Dirisha la Hifadhi ya Jamii Linalozingatia Sharia: Mafunzo kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF)."

Mdahalo huo ulifanyika wakati Tanzania Bara ikiwa bado haina taasisi inayotoa huduma za hifadhi ya jamii kwa mfumo wa Kiislamu, licha ya kukua kwa sekta nyingine za fedha za Kiislamu kama benki za Kiislamu, takaful na sukuk.

Mratibu wa CIFCA, Jumanne Bundala, alisema mdahalo huo ulilenga kuibua mjadala kuhusu haja ya kuanzisha madirisha maalumu au taasisi kamili za hifadhi ya jamii zinazofuata misingi ya Kiislamu ili kuongeza ujumuishi wa kifedha na ulinzi wa kijamii.

Mzungumzaji Mkuu katika hafla hiyo alikuwa ni Abdulazizi Eidi, Mkurugenzi wa Kitengo cha Shariah katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), ambaye alisema moja ya changamoto kubwa ni uelewa mdogo wa jamii kuhusu uwezekano wa kuwa na hifadhi ya jamii inayofuata misingi ya Kiislamu.

"Kwa baadhi ya watu ni jambo geni kusikia kwamba hata huduma za hifadhi ya jamii zinaweza kutolewa kwa misingi ya Kiislamu. Ndiyo maana uelewa, elimu na mawasiliano ni muhimu sana," alisema.

Aliipongeza CIFCA kwa kuanza kujenga mjadala huo na kuitaka taasisi hiyo kuendelea kuwafikia wadau mbalimbali, wakiwemo watunga sera, taasisi za hifadhi ya jamii na jamii kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Eidi, mabadiliko yanaweza kuanzia juu kupitia maamuzi ya serikali au taasisi zenye mamlaka, lakini pia yanaweza kuanzia chini pale wanachama wa mifuko wanapoanza kudai huduma zinazokidhi misingi yao ya dini.

"Wanachama wakitambua kwamba huduma hii inawezekana, wanaweza kupeleka mapendekezo yao kwenye taasisi husika na mabadiliko yakaanza," alisema.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kujenga uwezo kwa wasimamizi wa sekta, maafisa wa mifuko na wanazuoni wa Sharia ili waweze kuelewa vizuri namna mifumo hiyo inavyofanya kazi.

Katika hatua nyingine, Eidi alieleza umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika mifumo ya fedha za Kiislamu ili kuongeza uwazi, ufanisi na imani ya jamii.

Alitoa mfano wa mfumo mmoja wa kidijitali uliowezesha wafadhili kuchangia moja kwa moja kupitia simu kutoka mataifa mbalimbali, huku wakipata taarifa za matumizi ya michango yao kwa uwazi.

"Kwa kutumia mifumo ya kidijitali, mtu akiwa Saudi Arabia au Pakistan anaweza kuchangia kwa simu yake na kuona taarifa zote za namna mchango wake ulivyotumika. Hii inaongeza uwazi na kujenga imani," alisema.

Eidi pia alisisitiza umuhimu wa taasisi za Kiislamu, ikiwemo benki za Kiislamu, kampuni za takaful na mifuko ya kijamii kushirikiana kwa karibu zaidi ili kurahisisha utoaji wa huduma na miamala.

"Tunahitaji ushirikiano, kujitoa na uwajibikaji. Tukifuata misingi ya Kiislamu vizuri katika huduma hizi, jamii inaweza kunufaika zaidi kiuchumi na kijamii," alisema.

Washiriki wa mdahalo huo walieleza matumaini kuwa Tanzania inaweza kujifunza kutoka Zanzibar na nchi nyingine zilizoanza mifumo hiyo, huku wakiamini kuwa huduma za hifadhi ya jamii zinazozingatia Sharia zinaweza kusaidia kuongeza ushiriki wa wananchi katika sekta rasmi za kifedha.

ذو الحجة

HABARI ZANZIBAR

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Rais Mwinyi: Sina nia kuongezewa muda wa uongozi, miaka 10 yatosha



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, amesema hana nia ya kuongeza muda wa Urais zaidi ya muda uliowekwa kikatiba na kuagiza kusitishwa mara moja kwa mijadala kuhusu suala hilo.

Dkt. Mwinyi amesema kupitia majukwaa mbalimbali, ikiwemo Baraza la Wawakilishi, kumekuwa na mijadala na mapendekezo ya kuongeza muda wa Urais badala ya miaka 10 iliyowekwa na Katiba ya Zanzibar, lakini amesisitiza kuwa hana dhamira hiyo na kwamba mjadala huo hauna tija kwa nchi kwa sasa.

Amesema viongozi wameapa kuilinda Katiba ya Nchi na kuwataka wananchi na viongozi kuelekeza nguvu katika utekelezaji wa maendeleo ya taifa. Ameeleza kuwa kipindi kilichobaki cha uongozi wake kitakuwa cha utekelezaji mkubwa na wa kasi zaidi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla.

Rais Dkt. Mwinyi ameyasema hayo alipofungua Jukwaa la Wenyeviti na Wakuu wa Taasisi za Umma lililofanyika katika Hoteli ya Golden Tulip Airport, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Wakati huo huo, Rais Dkt. Mwinyi amesema Serikali haitakuwa tayari kuendelea kubeba mashirika ya umma yanayoshindwa kujiendesha na kuendelea kutegemea ruzuku kutoka Serikalini.

Amesema bado yapo mashirika ya umma yanayolipwa mishahara na kuendeshwa kwa fedha za Serikali jambo alilosema limepitwa na wakati, huku akiitaka taasisi hizo kujipanga na kujiendesha kwa tija na faida.

Halikadhalika D kt. Mwinyi amesema Serikali itatoa muda kwa mashirika hayo kufanya mageuzi ya kiutendaji na yale yatakayoshindwa kujiendesha Serikali haitakuwa tayari kuendelea nayo.

Vilevile Dkt. Mwinyi amesisitiza kuendelea kwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2050 pamoja na miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo ujenzi na uimarishaji wa bandari, viwanja vya ndege, viwanja vya michezo na miundombinu ya barabara ili kuifanya Zanzibar kuwa kitovu cha uchumi wa kisasa na endelevu.

ذُو الْحِجَّة

MAKALA ZA WAQFU

NA IDARA YA ELIMU YA AQWAF TANZANIA

# Dhulma dhidi ya waqfu: makosa makuu na hatari ya kupotea kwa amana za Allah Tanzania

**Mali ya Waqfu katika Uislamu ni sadaka yenye kuendelea (Sadaka Jariyah) ambayo mtoaji huitegemea imsaidie kaburini na Siku ya Malipo. Hata hivyo, nchini Tanzania, dhana hii takatifu inakabiliwa na changamoto za kimfumo zinazotishia kufuta kabisa manufaa yake kwa jamii. Changamoto hizi zimejikita katika utoaji, usimamizi, na matumizi ya mali za Waqfu. Makala hii inachambua makosa makuu matatu katika Amana za Waqfu.**

## Makosa katika utoaji

Utoaji wa kisiri bila maandishi au mashahidi

Kosa kubwa la watoaji wengi ni kutoa mali za Waqfu bila nyaraka rasmi za kisheria (Waqfiyyah). Wengi hutegemea "kauli ya mdomo" pekee. Mfano, mzee mmoja anatoa kiwanja chake Kariakoo kuwa Waqfu kwa ajili ya msikiti, lakini haandikishi popote. Anapofariki, watoto wake — wasio na hofu ya Allah — wanakigeuza kuwa mali ya urithi na kuanza kukiuza.

Kiini cha tatizo hapa ni kutokuwepo kwa maandishi wala mashahidi, mara nyingi kutokana na usiri. Allah Mtukufu anatuamuru kuandika mikataba na amana: "Enyi mlioamini, Mnapopeana deni (au amana) kwa muda maalumu, basi liandikeni..." [Quran, 2: 282].

Hivyo, kutoandika Waqfu ni kosa la kisheria na linalofungua mlango wa dhulma.

## Wasimamizi wenye tamaa

Hata hivyo, tatizo halipo tu kwa wale wasioweka maandishi. Wapo pia watoaji wanaoacha nyaraka halali kabisa za Waqf, lakini baada ya wao kufariki au kudhoofika, baadhi ya wasimamizi au warithi —kwa tamaa ya kujinufaisha na kukosa hofu ya Allah — hubadilisha makusudio ya Waqfu au hata kutaifisha mali hizo na kuzifanya miliki zao binafsi.

Hali hii imesababisha kuwepo kwa migogoro mingi inayofikishwa mahakamani, jambo linalodhoofisha dhamira na heshima ya Waqfu katika jamii.

## Makosa katika usimamizi

## Mikataba ya Kifisadi

Wasimamizi wengi (Mutawalli) wamegeuza mali za Waqfu kuwa fursa ya kujitajirisha badala ya kuzilinda.

Mfano, katika mikoa ya Tanga na Dar es Salaam, majengo ya Waqfu yaliyo katikati ya majiji hayo yanapangishwa kwa Sh 200,000 kwa mwezi, ilhali thamani ya soko ni Sh 1,500,000.

Msimamizi hupokea "kodi kwa siri" kutoka kwa mpangaji na kuingiza kiasi kidogo kwenye taasisi. Hii ni khiyana ya wazi kwa amana ya Allah.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Kila mmoja wenu ni mchungaji, na kila mmoja ataulizwa juu ya kile alichokichunga..." [Bukhari na Muslim]. Hivyo, nafasi ya usimamizi ni amana nzito; na bila uadilifu, inaweza kuwa sababu ya adhabu.

## Makosa katika matumizi

## Kutelekeza vipaumbele vya jamii

Kuna matumizi yasiyo na tija au yanayokwenda kinyume na nia ya mtoa Waqfu. Mfano huko Mwanza, ardhi ya Waqfu imekaa zaidi ya miaka 30 bila kuendelezwa, huku jamii ikikosa huduma muhimu kama zahanati au madrasa ya kisasa.

Kutelekeza mali bila kuizalisha ili kusaidia wenye uhitaji ni kosa kubwa la kiutawala. Allah Mtukufu anasema: "Enyi mlioamini, Msimkhini Mwenyezi Mungu na Mtume, wala msizikhini amana zenu hali ya kuwa mnajua." [Quran, 8: 27].

Kosa jingine ni kutumia mapato ya Waqfu kwa safari au posho za viongozi badala ya kusaidia walengwa.

## Upendeleo kwa ndugu, marafiki

Kosa la jingine ni upendeleo katika usimamizi ambapo baadhi ya wasimamizi hutoa upendeleo kwa ndugu au marafiki katika upangishaji, ajira, au utoaji wa zabuni za Waqfu.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Yeyote atakayepewa kazi na sisi, kisha akaficha hata sindano, atakuja nayo Siku ya Qiyama akiwa ameibeba." [Muslim]. Hata matumizi madogo yasiyo halali ni mzigo mkubwa mbele ya Allah.

## Njia za kurekebisha makosa haya

Kuna njia kadhaa za kurekebisha makosa haya. Kwanza, ni lazima kujielimisha kuhusu dhana ya Waqfu na kuimarisha uadilifu kwa wahusika wote, kuanzia watoaji hadi wasimamizi.

Watoaji wanapaswa kusisitizwa kuandikisha mali zao kwa wanasheria na mamlaka husika, hususan taasisi za Awqaf Tanzania.

Pili, ufanyike ukaguzi wa nje (External Audit) wa mara kwa mara ili kudhibiti upotevu wa mapato. Sambamba na hilo, kuwepo na mifumo ya kidijitali (E-Waqf) itakayoweka wazi taarifa za mali zote za Waqfu, -ikiwemo eneo, thamani, mapato, na mikataba- ili kuongeza uwazi kwa jamii.

Aidha, ni muhimu kuimarisha ulinzi wa kisheria wa nyaraka za Waqfu ili kuzuia mabadiliko haramu ya madhumuni au umiliki wake. Migogoro ya mara kwa mara mahakamani ni ishara kuwa hatua madhubuti za kisheria na kiutawala zinahitajika haraka.

Aidha, ni muhimu kuboresha mali za Waqfu kwa kuziongezea thamani ili ziwe na tija endelevu. Maboresho haya yanapaswa kugusa maeneo manne: kiutawala, kiuchumi, kisheria, na kiteknolojia.

## Hitimisho

Waqfu ni njia ya kuelekea Peponi kwa mtoaji, lakini inaweza kuwa sababu ya adhabu kwa msimamizi dhalimu au yeyote anayebadili makusudio yake kwa tamaa binafsi. Tanzania inaweza kupiga hatua kubwa kiuchumi na kijamii iwapo tutalinda na kuendeleza ipasavyo amana hii tukufu ya Allah. Allah atuongoze kuepuka makosa haya makubwa na mengine madogo.

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Mikakati ya Serikali kudhibiti upandaji holela bei za bidhaa

Serikali imesema itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha kupanda kwa bei za mafuta duniani hakuendelei kuwa mzigo kwa wananchi, huku ikionya wafanyabiashara wanaotumia hali hiyo kuongeza bei za bidhaa kiholela bila kuzingatia uhalisia wa gharama za uzalishaji na usafirishaji.

Kauli hiyo imekuja wakati ambao Watanzania wameendelea kukabiliwa na ongezeko la gharama za maisha kama vile kupanda kwa nauli, gharama za usafirishaji wa mizigo na bei za bidhaa muhimu ikiwamo vyakula.

Katika kipindi hicho, bei za mafuta nchini zimefikia zaidi ya Sh4,000 kwa lita, jambo linalowafanya baadhi ya watu kuanza kutafuta njia mbadala za kupunguza matumizi ya mafuta, ikiwamo kufunga mifumo ya gesi asilia kwenye magari.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Profesa Kitila Mkumbo, katika mkutano wa wadau kuhusu mashauriano kuhusu athari za mabadiliko ya bei ya mafuta duniani.

Alisema Serikali haiwezi peke yake kubeba mzigo wa changamoto hiyo kupitia ruzuku au kupunguza tozo bila ushirikiano wa wadau wengine wa uchumi.

Profesa Kitila, alisema ni muhimu kwa sekta binafsi kushiriki katika kuhakikisha bei za bidhaa zinapangwa kwa uwajibikaji, huku wakiboresha ufanisi wa minyororo ya ugavi na kuwekeza katika ubunifu utakaopunguza gharama za usafirishaji.

“Ndiyo maana tunahitaji ushirikiano wa jamii nzima, si Serikali pekee. Sekta binafsi ina wajibu mkubwa kuhakikisha inawajibika kupanga bei, kuboresha ufanisi wa minyororo ya ugavi na kuwekeza katika ubunifu unaopunguza gharama za uzalishaji na usafirishaji,” alisema.

Alisema Serikali haitarajii kuona wafanyabiashara wakitumia mgogoro huo kama sababu ya kuongeza bei kiholela kwa bidhaa ambazo hazijaathiriwa moja kwa moja na gharama za mafuta.

“Hatutarajii wafanyabiashara kutumia mgogoro huu kama kisingizio cha kuongeza bei kiholela. Kwa sababu sasa hata bei ya baiskeli inapopanda, ukiuliza kwa nini wanaongeza bei, wanajibu ni kwa sababu ya mgogoro wa Iran, si sawa,” alisema.

Kutokana na hali hiyo, amezitaka mamlaka za udhibiti nchini kuongeza uwazi katika soko pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa bei ili kuzuia vitendo vya unyonyaji dhidi ya wananchi.

Mbali na hatua za muda mfupi, alisema Serikali imeanza kufikiria mikakati ya muda wa kati na mrefu, itakayosaidia kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nchi chache.

Alisema Serikali pia itaendelea kushirikiana na nchi za Afrika Mashariki katika uwekezaji wa miundombinu ya kusafisha mafuta ndani ya ukanda huo ili kupunguza utegemezi.

“Hata nchi zinazozalisha mafuta bado husafirisha mafuta ghafi nje ya Afrika. Hivyo mgogoro huu unatukumbusha umuhimu wa kuwekeza zaidi katika viwanda vya kusafisha mafuta ndani ya bara letu,” alisema.

Profesa Kitila, alisema mjadala mpya umeanza kuhusu uwezekano wa kujengwa kwa kiwanda cha kusafisha mafuta Tanga au Mombasa nchini Kenya, hatua inayolenga kuongeza usalama wa nishati hiyo Afrika Mashariki.

Aidha, alisema hali hiyo imeonyesha umuhimu wa kuimarisha biashara ndani ya Afrika kupitia Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA), akisisitiza bara hilo lina uwezo wa kuwa kitovu cha biashara ya nishati, endapo litawekeza katika miundombinu na uzalishaji.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk Tausu Kida alisema tathmini ya kitaalamu inaonyesha kuna maeneo matatu muhimu yanayohitaji uangalizi wa karibu katika kipindi kilichopo.

Alitaja eneo la kwanza ni ufuatiliaji wa viashiria vya uchumi kama bei za mafuta, chakula, upatikanaji wa mbolea, gharama za usafirishaji, mwenendo wa ubadilishaji fedha na ustawi wa kaya.

Pili, alisema kuna umuhimu wa kuunganisha hatua za haraka za kupunguza madhara ya kiuchumi na mageuzi ya muda wa kati yatakayosaidia kuimarisha uzalishaji wa ndani, mifumo ya usafirishaji na usalama wa nishati.



ذو الحجة

## KUTOKA KWA MAJIRANI

UKHTI FATIMA SS

# Mivutano ya hijab mashuleni Kenya yaibua mjadala wa uhuru wa dini



Mivutano kuhusu wanafunzi wa Kiislamu kuvaa hijab katika shule zinazodhaminiwa na makanisa nchini Kenya imeibua upya mjadala kuhusu uhuru wa dini na haki ya elimu nchini humo, umeripoti mtandao wa habari wa Religion unplugged.

Mjadala huo umechochewa na tukio la mwanafunzi Samira Ramadhan, mwenye umri wa miaka 15, aliyelazimika kuhamia shule nyingine baada ya kuambiwa aondoe hijab katika shule ya St. Mary's Lwak Girls High School, kaunti ya Siaya.

Tukio hilo lilijadiliwa hata bungeni, ambapo wabunge walihoji hatua ya shule hiyo na kuitaja kama ubaguzi wa kidini.

Serikali kupitia Katibu Mkuu wa Elimu ya Msingi, Julius Bitok, baadaye iliamuru mwanafunzi huyo arudishwe shuleni mara moja.

Matukio kama hayo pia yameripotiwa Mombasa na Kitui, ambapo viongozi wa Kiislamu walizishutumu baadhi ya shule za Kikristo kwa kuwazuia wanafunzi wa Kiislamu kuvaa hijabu au kuwashinikiza kushiriki ibada za Kanisa Katoliki.

Ingawa takriban asilimia 20 ya wanafunzi nchini Kenya husoma katika shule binafsi, mjadala huu ni mpana zaidi kwa sababu shule nyingi za misheni haziwezi kuchukuliwa kama taasisi binafsi kwa maana halisi.

Nyingi zilijengwa katika ardhi ya umma, hupokea fedha za serikali, huajiri walimu kupitia Tume ya Huduma za Walimu — taasisi ya serikali — na hupokea wanafunzi kupitia mfumo wa kitaifa wa upangaji wanafunzi.

Hivyo, wakosoaji wanasema shule hizo zinapowazuia wanafunzi wa Kiislamu kuvaa hijab, suala hilo linagusa moja kwa moja wajibu wa serikali kulinda haki ya elimu na uhuru wa dini.

Waislamu nchini Kenya wanasema hijab si vazi la kawaida bali ni sehemu ya ibada, hivyo kuwazuia wanafunzi kuivaa ni sawa na kuwanyima haki ya elimu kwa misingi ya dini.

Hata hivyo, shule zinazomilikiwa au kudhaminiwa na makanisa zinasema wanafunzi wanaojiunga katika taasisi hizo wanapaswa kuheshimu utamaduni na kanuni za shule husika.

Mzozo huo umeendelea kutokana na kukosekana kwa mwongozo rasmi wa serikali kuhusu mavazi ya kidini mashuleni, licha ya Mahakama ya Juu ya Kenya kuagiza serikali kuandaa mwongozo huo mwaka 2019.




HABARI DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Hofu ya vita yashindwa kuteteresha Hijja

Licha ya mvutano wa kisiasa na hofu ya kurejea kwa vita Mashariki ya Kati, zaidi ya mahujaji milioni 1.5 tayari wamewasili nchini Saudi Arabia kwa ajili ya ibada ya Hijja mwaka huu, jambo linaloonyesha namna imani ya kidini ilivyoendelea kushinda hofu ya usalama.

Miongoni mwao ni zaidi ya mahujaji 4,000 kutoka Tanzania ambao wameanza kuelekea Saudi Arabia kupitia makundi mbalimbali ya Hijja, huku viongozi wa dini nchini wakiwakumbusha kuwa safari hiyo si ya starehe bali ni ibada inayohitaji subra, nidhamu na unyenyekevu.

Mamlaka za Saudi Arabia zilisema hadi Ijumaa iliyopita mahujaji 1,518,153 kutoka nje ya nchi hiyo walikuwa tayari wameingia kwa ajili ya ibada hiyo kubwa ya Kiislamu, idadi ambayo tayari imezidi mahujaji wa kimataifa wa mwaka jana katika kipindi kama hiki.

Hijja, ambayo ni nguzo ya tano ya Uislamu, inaanza rasmi Jumatatu katika mji mtakatifu wa Makka. Kila Muislamu mwenye uwezo wa kifedha na kiafya anatakiwa kuitekeleza angalau mara moja katika maisha yake.

Mwaka huu ibada hiyo imefanyika katika mazingira ya taharuki kufuatia vita kati ya Iran kwa upande mmoja na Marekani pamoja na Israel kwa upande mwingine, hali iliyosababisha mashambulizi ya makombora, kufungwa kwa baadhi ya anga za nchi za Ghuba na usumbufu mkubwa wa safari za ndege.

Pamoja na hali hiyo, mahujaji kutoka mataifa mbalimbali wameendelea kuelekea Saudi Arabia kwa wingi wakieleza kuwa ibada hiyo ni mwito wa kiroho usioweza kuzuiwa na hofu ya vita.

Fadel, raia wa Marekani mwenye umri wa miaka 49 aliyeko Makka kwa Hijja, alisema hakuwa na shaka yoyote ya kufuta safari yake hata wakati vita vikiendelea.

"Hata kama vita vingekuwa vinaendelea bado nisingeahirisha Hijja," alinukuliwa akisema huku akisisitiza kuwa waumini wanaamini wako "mahali salama zaidi duniani."

Hisia kama hizo zimeonekana pia kwa Waislamu wengine kutoka nchi za Magharibi, licha ya baadhi ya serikali zao kutoa tahadhari za safari kuelekea Mashariki ya Kati.

Ubalozi wa Marekani mjini Riyadh uliwataka raia wake "kufikiria upya" kushiriki Hijja mwaka huu kutokana na hali ya usalama na uwezekano wa kuvurugika kwa safari za ndege.

Hata hivyo, Faisal Rashid, mwanafunzi wa shahada ya uzamivu kutoka California, alisema yeye na mkewe walijitahidi kwa nguvu kupata nafasi ya Hijja mapema mwaka huu kabla ya vifurushi kuisha.

Rashid alisema habari za vita zilimfanya kuwa makini zaidi katika kufuatilia safari na taarifa za usalama, lakini hazikubadilisha azma yake ya kwenda Hijja.

"Katika Uislamu tunafundishwa kufanya juhudi zetu zote kisha kumuachia Mungu mambo tusiyoweza kuyadhibiti," alisema.

Kwa mamilioni ya Waislamu, Hijja si safari ya kawaida ya kidini bali ni tukio kubwa la kiroho lenye kuhusishwa na msamaha wa dhambi, toba, unyenyekevu na umoja wa Waislamu duniani. Waumini huamini kuwa Hijja humsogeza Muislamu karibu zaidi na Mwenyezi Mungu huku ikiwa ni fursa ya kuanza maisha mapya ya kiroho.

Ibada hiyo pia huwakutanisha Waislamu wa mataifa, rangi, lugha na tabaka tofauti katika mazingira yanayoonyesha usawa na mshikamano wa Kiislamu. Wengi huondoka kwa miaka mingi wakijiwekea akiba ya fedha au wakingoja kibali ili kutimiza ndoto hiyo ya maisha.

Kwa Tanzania, viongozi wa taasisi za Hijja wameendelea kuwasisitiza mahujaji kujiandaa kimwili na kiroho kutokana na mazingira ya msongamano mkubwa wa watu katika maeneo matakatifu ya Makka, Mina na Arafa.

Hijja hufanyika katika mwezi wa Dhul-Hijjah wa kalenda ya Kiislamu, ambapo mahujaji hutekeleza mfululizo wa ibada katika siku kadhaa. Kabla ya kuingia Makka, mahujaji huingia katika hali ya ihram, ambapo wanaume huvaa mavazi meupe yasiyoshonwa kuashiria usawa, unyenyekevu na kuondoa tofauti za utajiri, utaifa au hadhi.

Mahujaji huingia Makka wakisoma talbiyah kwa wingi huku wakijitenga na mambo ya anasa na majivuno ya dunia.

Baada ya hapo huzunguka Al-Kaaba mara saba katika ibada ijulikanayo kama tawaf, kabla ya kutembea kati ya vilima vya Safa na Marwa wakikumbuka simulizi ya Hajjar, mke wa Nabii Ibrahim, aliyekuwa akitafuta maji kwa ajili ya mwanawe Ismail mpaka kisima cha Zamzam kilipopatikana.

Miongoni mwa ibada muhimu zaidi ni kusimama katika Uwanja wa Arafa, tukio ambalo wanazuoni wengi hulitaja kuwa "moyo wa Hijja." Katika siku hiyo mahujaji hutumia muda mwingi katika dua, toba na kuomba msamaha huku wengi wakibubujikwa na machozi.

Baadaye mahujaji hukusanya kokoto Muzdalifah na kuelekea Mina kutupa mawe katika nguzo zinazowakilisha kumpinga shetani na majaribu yake. Aidha, hufanya ibada ya kuchinja kama kumbukumbu ya utiifu wa Nabii Ibrahim kwa Mwenyezi Mungu.

Wanaume pia hunyoa au kupunguza nywele zao huku wanawake wakikata sehemu ndogo ya nywele kama ishara ya utakaso na mwanzo mpya wa kiroho.

Mbali na changamoto za kisiasa, Saudi Arabia imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa ili kuongeza usalama wa mahujaji na kurahisisha ibada hiyo.

Mamlaka ya Takwimu na Akili Unde ya Saudi Arabia (SDAIA) imesema mwaka huu imepanua matumizi ya mifumo ya akili unde (AI) katika kusimamia mikusanyiko ya watu, usafiri, huduma za afya na kutoa msaada wa lugha mbalimbali kwa mahujaji.

Teknolojia hizo zinajumuisha roboti zinazotoa maelekezo ya kidini na tafsiri za lugha mbalimbali, pamoja na mifumo inayofuatilia msongamano wa watu katika maeneo ya Mina, Arafa na Msikiti Mkuu wa Makka kwa wakati halisi.

Hatua hizo zimekuja baada ya Saudi Arabia kukumbwa na ukosoaji mwaka 2024 kufuatia vifo vya zaidi ya mahujaji 1,300 vilivyosababishwa kwa kiasi kikubwa na joto kali pamoja na baadhi ya mahujaji kutembea umbali mrefu bila vibali rasmi.

Wachambuzi wa masuala ya Mashariki ya Kati wanaonya kuwa kurejea kwa mapigano kunaweza kuathiri safari za mahujaji katika siku zijazo, lakini kwa sasa hali ya utulivu wa tahadhari imeendelea kuwepo.

Hata hivyo, kwa mahujaji wengi waliowasili Makka, imani imeonekana kuwa kubwa kuliko hofu.

Eid Al-Adha

**SHEIKH**
Shaaban Mussa
0786 272 323



# Swala ya Eid: Ibada ya furaha, umoja na kumshukuru Allah

## ■ Tuzingatie Sunna na adabu zake



501201344

# Swala ya Eid: Ibada ya furaha, umoja na kumshukuru Allah

**Swala ya Eid ni miongoni mwa ibada kubwa na alama muhimu za dini ya Kiislamu zinazowaunganisha Waislamu duniani kote katika siku za furaha, shukrani na ibada kwa Mwenyezi Mungu.**

**Katika Uislamu, kuna sikukuu mbili kuu ambazo ni Eid al-Fitr na Eid al-Adh-haa. Sikukuu hizi zimewekwa kwa mujibu wa Qur'an Tukufu, Sunna za Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) pamoja na makubaliano ya wanazuoni wa Kiislamu.**

**Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) alipofika Madina aliwakuta watu wakiwa na siku maalumu za michezo na sherehe walizorithi tangu zama za ujahiliya.**

**Hata hivyo, aliwaeleza kuwa Mwenyezi Mungu amewabadilishia siku bora zaidi ambazo ni Eid ya Fitri na Eid ya Adh-haa.**

**Wanazuoni wanaeleza kuwa Eid imeitwa kwa jina hilo kwa sababu hurudi kila mwaka ikiwa ni ishara ya furaha, rehema na neema kutoka kwa Allah baada ya utekelezaji wa ibada kubwa kama kufunga mwezi wa Ramadhan na kuhiji.**

## Swala ya Idi, nembo ya Uislamu

Kwa mujibu wa mafundisho ya Kiislamu, Swala ya Eid ni miongoni mwa alama kubwa zinazoonesha mshikamano wa Waislamu.

Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliendelea kuiswali swala hiyo katika maisha yake yote, na Waislamu wakaendeleza sunna hiyo kizazi hadi kizazi.

Swala hiyo huswaliwa katika viwanja vya wazi au maeneo makubwa ya mikusanyiko ili kuonesha umoja wa Waumini na ukubwa wa Uislamu, isipokuwa katika Masjid al-Haram ambako Swala ya Eid huswaliwa ndani ya Msikiti Mtukufu.

## Wakati na namna ya kuswali

Swala ya Eid huswaliwa baada ya Jua kuchomoza na kupanda kiasi kidogo hadi muda mchache kabla ya adhuhuri. Swala hiyo ina rakaa mbili na haiswaliwi kwa adhana wala iqama.

Katika rakaa ya kwanza, kabla ya kusoma Qur'an, husomwa takbira za ziada sita baada ya takbira ya kuanzia, huku rakaa ya pili ikiwa na takbira tano.

Imam husoma Qur'an kwa sauti, na miongoni mwa sura zinazopendekezwa kusomwa ni Surat Al-A'laa na Al-Ghaashiyah, au Surat Qaaf na Al-Qamar. Baada ya Swala hutolewa khutba maalumu yenye mawaidha, nasaha na mafundisho kuhusu masuala ya dini na jamii.

Mafundisho ya Kiislamu pia yanawahimiza wanawake kuhudhuria Swala ya Eid kwa kuzingatia maadili na stara za Kiislamu. Wanawake wanatakiwa kuhudhuria bila kujitia manukato au kuvaa mavazi ya kujionesha. Hata wanawake wenye hedhi wanaruhusiwa kushuhudia mkusanyiko wa Waislamu na kushiriki dua za siku hiyo.

## Sunna za siku ya Eid

Miongoni mwa mambo yanayopendekezwa katika siku ya Eid ni kuoga, kuvaa nguo nzuri na safi, pamoja na kuwahi kwenda kwenye Swala ya Eid.

Kwa Eid ya Fitri, Muislamu anashauriwa kula tende kwa idadi ya witri kabla ya kutoka kwenda kuswali, huku kwa Eid ya Adh-haa ikipendekezwa kutokula mpaka baada ya Swala.

Aidha, ni Sunna kwenda kwenye Swala kwa njia moja na kurudi kwa njia tofauti pamoja na kupaza sauti za takbira kwa wanaume.

Takbira zinazopendekezwa ni: "Allahu Akbar, Allahu Akbar, Laa ilaaha illa Allah, Allahu Akbar Allahu Akbar wa lillaahil hamd."

## Tahadhari dhidi ya maovu siku ya Eid

Pamoja na furaha ya siku ya Eid, Waislamu wameonywa kujiepusha na mambo yanayokwenda kinyume na maadili ya Kiislamu kama muziki haramu, kuchanganyika kiholela kati ya wanaume na wanawake, mavazi yasiyo ya stara na starehe zinazochochea maasi.

Wanazuoni wamehimiza familia za Kiislamu kuitumia siku hiyo kwa ibada, kuimarisha undugu, kusaidiana na kufanya mambo yenye manufaa kwa jamii.

Kwa ujumla, siku ya Eid hubeba ujumbe mkubwa wa mshikamano, furaha na kumshukuru Mwenyezi Mungu. Waislamu wamehimizwa kuitumia siku hiyo kuendeleza upendo, kutembeleana na kuombeana mema kwa kauli maarufu isemayo: "Taqabbalallahu minna wa minkum" (Mwenyezi Mungu atukubalie mema yetu na yenu).

***Na Allah ndiye Mjuzi zaidi***



Eid Al-Adha

KUTOKA KWA MHARIRI

Mhariri
0789 201383

# Eid al–Adh'ha ni siku ya ibada, siyo maasi

Eid al–Adh'ha ni miongoni mwa alama tukufu za Uislamu na siku muhimu kwa Waislamu duniani kote. Hata hivyo, kila zinapowadia siku za Eid, baadhi ya watu hujihusisha na vitendo vinavyomkasirisha Mwenyezi Mungu badala ya kutumia siku hizo katika ibada na matendo mema.

Baadhi ya watu hujihusisha na ulevi, muziki, matumizi mabaya ya fedha pamoja na tabia nyingine zinazokwenda kinyume na maadili ya Kiislamu. Mafundisho ya Uislamu yanaeleza kuwa Eid ni siku ya kula, kunywa na kumdhukuru Mungu.

Pia ni siku ya kuwatembelea ndugu, jamaa, marafiki pamoja na kuwasaidia wenye uhitaji kama vile masikini, mayatima, wenye ulemavu na wafungwa ili nao washiriki furaha ya siku hiyo.

Hivyo, Eid imekusudiwa kuwa siku ya mshikamano, huruma na kusaidiana, si siku ya kufanya maasi. Hakika, siku za Eid ni siku za furaha kwa mwenye nia njema na anayemshukuru Allah kwa neema zake.

Allah Mtukufu anasema: "Na anayetukuza ibada za Allah, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo." [Qur'an, 22:32]. Aya hii inaonesha umuhimu wa kuheshimu alama za dini na kuziadhimisha kwa namna inayomridhisha Muumba.

Katika Uislamu, sikukuu ni sehemu ya ibada kwa sababu zimefungamana na ibada mbalimbali. Ndani yake hudhihiri tabia njema kama upendo, huruma, kusaidiana na mshikamano wa Kiislamu.

Eid ni siku ya kuwatembelea wenye shida, kuwafariji na kuwapa matumaini. Pia ni wakati wa kutakasa nafsi kutokana na udanganyifu na matamanio mabaya ya shetani. Pamoja na hayo, Uislamu haukatazi kufurahia neema za Allah kwa kula vizuri, kuvaa vizuri na kusherehekea kwa kuzingatia mipaka ya dini.

Ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya vijana na watu wazima wakitumia siku za Eid kufanya matendo yasiyoendana na maadili ya Kiislamu.

Eid si siku ya kujifaharisha kwa mavazi mapya, kujionesha kwa kiburi, wala kujikusanya katika fukwe za bahari, wanaume na wanawake pamoja katika mandhari zilizoharamishwa katika dini. Vitendo hivyo huondoa baraka za siku hii tukufu na kuifanya ipoteze maana yake halisi.

Muislamu anatakiwa kuwa mnyenyekevu, mwenye shukrani na anayezingatia wajibu wake kwa Allah na kwa jamii inayomzunguka. Furaha ya kweli katika Eid hupatikana kwa kufanya ibada, kutoa sadaka na kuwafurahisha wenye mahitaji.

Uislamu unamtaka Muislamu awe na haiba yake tofauti na wasiokuwa Waislamu katika namna ya kusherehekea sikukuu.

Mtume Muhammad (Allah amshushie rehema na amani) ameonya dhidi ya kuiga desturi zinazopingana na mafundisho ya dini. Hivyo, ni wajibu wetu kutumia sikukuu ya Eid al–Adh'ha kwa ibada, toba, mshikamano na matendo mema. Tumuombe Allah awahurumie wenye shida, wagonjwa, wafungwa na masikini ili nao wapate furaha ya siku hii.



## HABARI ZANZIBAR

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Marekani yaonywa isianzishe vita siku za ibada ya Hijja




Saudi Arabia imeripotiwa kuiomba serikali ya Rais Donald Trump kuepuka mashambulizi makubwa dhidi ya Iran hadi baada ya msimu wa Hijja wa mwaka huu, huku nchi za Ghuba zikihofia kuongezeka kwa mvutano wa kijeshi wakati mamilioni ya Waislamu wakijiandaa kuelekea Makka.

Kwa mujibu wa taarifa zilizochapishwa na The New Arab, viongozi wa Saudi Arabia pamoja na mataifa mengine ya Ghuba wameiomba Washington kutoa nafasi kwa juhudi za kidiplomasia badala ya kuanzisha mashambulizi mapya katika kipindi cha Hijja.

Mwaka huu Hijja inatarajiwa kuanza Mei 24 na kuhudhuriwa na zaidi ya mahujaji milioni 1.5 kutoka duniani kote.

Ripoti zinaeleza kuwa viongozi wa Ghuba wana hofu kuwa Iran inaweza kujibu mashambulizi yoyote kwa kulenga maeneo jirani, jambo ambalo linaweza kusababisha vurugu kubwa na kuwakwaza mahujaji pamoja na usafiri wa anga katika eneo hilo.

Maafisa wa Ghuba pia wameonya kuwa mashambulizi katika kipindi kinachoelekea Sikukuu ya Eid al-Adha yanaweza kuharibu zaidi taswira ya Marekani katika ulimwengu wa Kiislamu. Mvutano huo unakuja wakati juhudi za mazungumzo kati ya Iran na Marekani zikiendelea huku kukiwa na hofu ya kurejea kwa mapigano makubwa katika Mashariki ya Kati.

Eid Al-Adha

HABARI ZANZIBAR

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Hijja yaendelea licha ya mvutano Mashariki ya Kati



Licha ya mvutano wa kivita unaoendelea Mashariki ya Kati na ongezeko kubwa la gharama za usafiri, zaidi ya mahujaji milioni 1.5 wanaendelea na ibada ya Hijja mwaka huu katika mji mtakatifu wa Makka, Saudi Arabia.

Serikali ya Saudi Arabia imeendelea kusimamia ibada hiyo kwa usalama mkubwa huku Waislamu kutoka mataifa mbalimbali wakisisitiza kuwa Hijja ni wajibu wa kiimani usiozuiliwa na hofu ya vita wala changamoto za kiuchumi.

Taarifa mbalimbali zinaonesha kuwa katika kipindi cha zaidi ya miaka 1,400, ibada ya Hijja imesimamishwa au kupunguzwa mara chache sana, hali inayodhihirisha nafasi yake kubwa katika maisha ya Waislamu duniani.

Indonesia pekee imetuma zaidi ya mahujaji 221,000 mwaka huu, huku Iran ikitarajiwa kuwa na mahujaji wapatao 30,000 licha ya kuwa katikati ya mvutano wa kisiasa katika ukanda huo. Mahujaji wengi wa hali za kawaida wanaojilipia hujiandaa kwa safari hiyo kwa maisha yao yote, wakidunduliza fedha ili kutimiza nguzo hiyo muhimu.

Kupanda kwa bei ya mafuta ya ndege, bima za safari pamoja na mabadiliko ya njia za anga kutokana na vita, kumeongeza gharama za Hijja katika mataifa mengi.

Nchini India baadhi ya mahujaji wameongezewa zaidi ya dola 100 za Marekani kwenye gharama zao, huku serikali za Indonesia na Malaysia zikichukua hatua kusaidia gharama hizo ili kuhakikisha Waislamu hawanyimwi fursa ya kutekeleza ibada hiyo takatifu.

Katika kuimarisha usalama wa maeneo matakatifu, Saudi Arabia imeweka mifumo ya kisasa ya ulinzi wa anga, ikiwemo makombora ya aina ya Patriot na teknolojia za kuzuia droni karibu na Makka na Madina. Hatua hiyo imepokelewa vyema na Waislamu wengi duniani wanaoamini kuwa pamoja na migogoro ya kisiasa na vita vya kikanda, ibada ya Hija itaendelea kuwa alama ya umoja, subira na mshikamano wa Umma wa Kiislamu duniani.

Eid Al-Adha

HABARI ZANZIBAR

NA MAHMOUD NYAMGUMA

# Saudi Arabia yaonya Hijja isitumike kinyume na ibada

Saudi Arabia imesisitiza kuwa haitaruhusu msimu wa Hijja kutumiwa kwa shughuli zozote zinazokiuka madhumuni yake ya kidini, wakati zaidi ya mahujaji milioni 1.5 kutoka nje ya nchi tayari wamewasili kwa ajili ya ibada hiyo takatifu.

Akizungumza katika mkutano wa makamanda wa usalama wa Hijja mjini Makka, Mkuu wa Usalama wa Umma na Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama wa Hijja, Luteni Jenerali Mohammed Al-Bassami, alisema vyombo vya usalama viko tayari kikamilifu kuhakikisha mahujaji wanafanya ibada zao kwa usalama na utulivu.

Al-Bassami alisema mamlaka zimefanikiwa kuvunja zaidi ya kampeni 217 bandia za Hijja kote nchini na kuwazuia watu 7,733 waliokuwa wakijaribu kuingia Makka kinyume cha sheria.

Aidha, watu wasiopungua 366,000 ambao hawakuwa na vibali rasmi vya Hijja walizuiwa katika vituo vya kuingia Makka, huku maelfu ya magari yaliyokuwa yakitumika kusafirisha watu hao yakikamatwa.

Mamlaka za Saudi Arabia zimesema matumizi ya teknolojia za kisasa na mifumo ya akili bandia yanaendelea kusaidia kusimamia mikusanyiko mikubwa ya watu na kubaini ukiukwaji wa sheria haraka.

Kwa mujibu wa Idara ya Pasipoti, zaidi ya mahujaji milioni 1.518 kutoka nje ya Saudi Arabia walikuwa wamewasili kufikia Ijumaa alasiri.



NA MAHMOUD NYAMGUMA




# Mashambulizi dhidi ya Waislamu yaongeza hofu duniani

Wimbi la mashambulizi dhidi ya Waislamu na misikiti limeendelea kuibua hofu kubwa duniani huku matukio ya mauaji yakiongezeka katika mataifa ya Magharibi ikiwemo Marekani, Canada, Uingereza na New Zealand.

Tukio la hivi karibuni limetokea katika mji wa San Diego nchini Marekani ambapo watu watatu waliuawa kwa kupigwa risasi ndani ya Kituo cha Kiislamu cha San Diego, ikiashiria ongezeka la chuki dhidi ya Uislamu.

Takwimu za mashirika ya haki za binadamu yanaonesha ongezeko la mashambulizi kwa kasi katika muongo mmoja uliopita. Mwaka 2019, watu 51 waliuawa ndani ya misikiti miwili mjini Christchurch, New Zealand, katika moja ya mashambulizi mabaya zaidi dhidi ya Waislamu duniani.

Aidha mwaka 2017, Waumini sita waliuawa ndani ya msikiti wa Quebec City nchini Canada huku wengine wengi wakijeruhiwa baada ya mshambuliaji mwenye itikadi za mrengo mkali kufyatua risasi wakati wa swalah.

Propaganda za chuki dhidi ya Uislamu, ongezeko la siasa kali za mrengo wa kulia pamoja na ukimya wa baadhi ya serikali dhidi ya matamshi ya kibaguzi, vimechangia kuchochea mashambulizi hayo. Ripoti za kimataifa zinaonyesha kuwa matukio mengi ya ugaidi dhidi ya Waislamu yamehusishwa na itikadi za ubaguzi wa rangi na chuki dhidi ya wahamiaji wa Kiislamu katika nchi za Magharibi.

Jumuiya za Kiislamu duniani zimeendelea kuitaka jamii ya kimataifa kuchukua hatua madhubuti kulinda haki na usalama wa Waislamu, huku zikisisitiza kuwa kuendelea kwa

## Wahindu India wabaka binti wa miaka 14 kwa kuchukia Waislamu

**Jimbo la Uttar Pradesh nchini India limekumbwa tena na mjadala mkubwa wa ubaguzi dhidi ya Waislamu baada ya binti mwenye umri wa miaka 14 kudaiwa kubakwa na wanaume wa Kihindu katika wilaya ya Kannauj.**

**Binti huyo aliyekuwa akisoma katika madrasa ya Mohsinat alitoweka Mei 3 baada ya kudanganywa kuwa mama yake alikuwa akimuita, kabla ya kupatikana akiwa amefungiwa ndani ya nyumba moja karibu na madrasa hiyo huku akiwa katika hali mbaya kiafya.**

**Familia ya msichana huyo imeeleza kuwa watuhumiwa walimlazimisha kunywa kile kilichoelezwa kuwa pombe iliyofichwa kama soda kabla ya kumbaka kwa zamu, huku wakijaribu kuonesha kana kwamba aliolewa kwa hiari kwa kumpaka 'sindoor' kichwani na mahawar miguuni, alama zinazotumika katika mila za ndoa za Kihindu.**

**Sindoor ni unga wa rangi nyekundu au ya machungwa unaotumiwa na wanawake wa Kihindu kama ishara ya kuonyesha kuwa wameolewa.**

**Tukio hilo limezua hasira kubwa miongoni mwa jamii za Kiislamu ambazo zimekuwa zikilalamikia kuongezeka kwa mashambulizi, utekaji na ukandamizaji dhidi yao katika maeneo mbalimbali ya Uttar Pradesh chini ya serikali ya chama cha BJP.**

**Kwa mujibu wa taarifa za mashirika ya haki za binadamu nchini India, matukio ya chuki dhidi ya Waislamu yameongezeka katika miaka ya karibuni, huku ripoti za makundi ya kiraia zikionesha mamia ya visa vya vurugu, ubaguzi wa kidini na mashambulizi ya makundi ya wenye msimamo mkali wa Kihindu yakiripotiwa kila mwaka.**

**Wachambuzi wa masuala ya kijamii wanaeleza kuwa tukio la Kannauj ni sehemu ya mwenendo mpana unaoonesha namna mamlaka zinavyotuhumiwa kufumbia macho vitendo vya unyanyasaji dhidi ya Waislamu, hasa katika maeneo yenye historia ndefu ya migawanyiko ya kidini kama Uttar Pradesh.**

**Polisi wa Kannauj wamethibitisha kufunguliwa kwa kesi dhidi ya watuhumiwa hao huku mmoja akishikiliwa na wengine wakisakwa. Hata hivyo, wanaharakati wa Kiislamu nchini humo wanahoji kasi na uthabiti wa vyombo vya dola katika kushughulikia kesi zinazowahusu Waislamu, wakisema mara nyingi haki imekuwa ikicheleweshwa au kupuuzwa licha ya ushahidi mkubwa uliopo.**

**CHANZO: 5 Pillars**

# Majonzi, hofu kwa Waislamu nchi za Magharibi baada Shambulizi la msikiti San Diego

■ **Zaidi ya watu 2,000 wakusanyika kuomboleza watu waliouawa katika shambulio hilo**



# Majonzi, hofu kwa Waislamu nchi za Magharibi baada Shambulizi la msikiti San Diego

Shambulizi la kikatili lililotokea katika Kituo cha Kiislamu cha San Diego, California, na kuua watu watatu kabla washambuliaji wawili kujiua, limeacha majonzi makubwa kwa jamii ya Waislamu Marekani huku likifungua upya mjadala kuhusu kuongezeka kwa chuki za kidini na itikadi kali zinazochochewa mtandaoni.

Mashambulizi hayo yalitokea Mei 19, 2026 katika moja ya misikiti mikubwa zaidi ya San Diego, eneo ambalo pia lina shule ya Kiislamu yenye watoto zaidi ya 140. Kwa mujibu wa polisi na Shirika la Upelelezi la Marekani (FBI), washambuliaji hao wawili wenye umri wa miaka 17 na 18 walikuwa wamejengeka katika itikadi za ubaguzi wa wazungu kupitia mitandao ya mtandaoni.

Uchunguzi umeonesha kuwa washambuliaji hao walikuwa na maandishi yenye chuki dhidi ya Waislamu na makundi mengine, na kujitambulisha kama "Sons of Tarrant," wakirejea mshambuliaji wa Christchurch, New Zealand, aliyeua waumini 51 katika misikiti miwili mwaka 2019.

Kwa wengi ndani ya jamii ya Kiislamu Marekani tukio hilo ni ishara ya hatari kubwa zaidi: kuhalalishwa kwa chuki dhidi ya Waislamu katika mazingira ya kisiasa na mtandaoni.

NBC News imeripoti kuwa viongozi wa jamii ya Kiislamu San Diego wamesema walikuwa wameishi kwa miaka mingi chini ya vitisho, ujumbe wa chuki na hofu ya kushambuliwa, lakini hawakutarajia tukio kubwa kiasi hicho kutokea.

"Tumekuwa tukipokea ujumbe wa chuki kwa miaka, watu wakipita na kututukana. Lakini tukio kama hili hatukuwahi kufikiria," alisema Imam Taha Hassane wa kituo hicho.

Watu watatu waliouawa — Amin Abdullah, Mansour Kaziha na Nadir Awad — sasa wanatajwa kama mashujaa waliozuia mauaji makubwa zaidi kutokea.

Kwa mujibu wa mashuhuda na polisi, walijaribu kuwazuia washambuliaji hao kufika katika maeneo yaliyokuwa na watoto waliokuwa wakijificha ndani ya shule - kitendo kilichookoa maisha ya makumi ya watoto na walimu waliokuwa ndani ya jengo hilo.

Amin Abdullah, ambaye alikuwa mlinzi wa msikiti huo kwa zaidi ya miaka 10, alijibu mashambulizi hayo kwa kubadilishana risasi na washambuliaji huku akitoa tahadhari ya kufungwa kwa shule kupitia redio kabla ya kuuawa.

Kisa chake kimegusa wengi zaidi kutokana na historia yake ya kubadili dini kutoka Ukristo kwenda Uislamu miaka iliyopita baada ya kutafuta majibu kuhusu imani ya Mungu mmoja. Kabla ya kifo chake, alikuwa amewahi kueleza kuwa alihisi jukumu la kulinda waumini baada ya mashambulizi ya Christchurch.

NBC News imeripoti kuwa uhalifu wa chuki unaohusiana na dini umeongezeka kwa asilimia 150 San Diego kati ya mwaka 2024 na 2025. Wakati huo huo, Baraza la Mahusiano ya Kiislamu Marekani (CAIR) limesema lilipokea malalamiko 8,683 ya chuki dhidi ya Waislamu mwaka 2025 — idadi kubwa zaidi tangu mwaka 1996.

Wachambuzi wa masuala ya chuki na siasa wanaonya kuwa lugha kali dhidi ya makundi ya kidini au kikabila inapokuwa ya kawaida mtandaoni na katika siasa, huweza kuwafanya baadhi ya vijana wenye misimamo mikali kuona vurugu kama jambo la kawaida.

Hilo ndilo linalowatia hofu viongozi wengi wa dini Marekani: kwamba misikiti, masinagogi na nyumba nyingine za ibada zimeanza kuishi chini ya hali ya tahadhari ya kudumu.



Na UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# "Alisimama kati ya risasi na watoto": San Diego yaomboleza mlinzi shujaa wa msikiti

Ndani ya sekunde chache za hofu, Amin Abdullah alifanya uamuzi uliookoa maisha ya watoto wengi.

Siku ya Jumatatu, milio ya risasi iliposikika nje ya Kituo cha Kiislamu cha San Diego nchini Marekani, Abdullah — mlinzi wa msikiti huo — hakukimbia kujiokoa. Badala yake, aliwatahadharisha walimu na wanafunzi wafunge madarasa haraka, kisha akasimama uso kwa uso dhidi ya washambuliaji wawili waliokuwa wamejihami kwa bunduki.

Kwa mujibu wa polisi wa San Diego na viongozi wa msikiti huo, hatua yake iliwazuia washambuliaji hao kuwafikia zaidi ya watoto 140 na wafanyakazi waliokuwa ndani ya shule ya Kiislamu iliyopo karibu kabisa na msikiti huo.

Abdullah aliuwawa katika mapambano hayo ya risasi. Lakini jamii ya Waislamu wa San Diego inasema alikufa kama shujaa.

"Bila yeye, leo tungekuwa tunazungumzia mauaji ya watoto wengi," alisema Mkuu wa Polisi wa San Diego, Scott Wahl.

Mbali na Abdullah, wanaume wengine wawili — Mansour Kaziha na Nadir Awad — pia waliuwawa walipojaribu kuwavuta washambuliaji mbali na jengo la shule.

Kaziha, mwenye miaka 78, alikuwa sehemu ya msikiti huo tangu mwaka 1986. Alikuwa fundi, mpishi, mhudumu na mtu ambaye karibu kila mmoja katika msikiti alimjua. Awad, ambaye mke wake ni mwalimu katika shule hiyo, alikimbilia eneo la tukio mara aliposikia risasi kutoka nyumbani kwake jirani na msikiti.

Lakini simulizi iliyogusa wengi zaidi ni ya Abdullah.

Binti yake, Hawaa Abdullah, alisema baba yake alikuwa rafiki yake mkubwa na mfano wa maisha yake. Akiwa analia mbele ya wanahabari, alisema baba yake alikuwa akichukua kazi ya kulinda msikiti kwa uzito mkubwa kiasi kwamba wakati mwingine alikuwa akiogopa hata kwenda kula chakula, akihofia "kitu kibaya kinaweza kutokea akiwa mbali."

Abdullah alikuwa baba wa watoto wanane na alikuwa ameukubali Uislamu akiwa kijana baada ya kuvutiwa na mafundisho ya kumpwekesha Mungu.

Waliomfahamu wanasema alikuwa mtu mwenye tabasamu la kudumu, aliyewakaribisha watu msikitini kwa upole na heshima. Lakini siku ya shambulizi, aligeuka kuwa ngao ya watoto.




"Mimi naamini kabisa moyoni mwangu kuwa alikubali kufa ili watoto wa watu wengine waendelee kuishi," alisema mmoja wa wazazi wa shule hiyo.

Mamia ya watu wameendelea kukusanyika nje ya msikiti huo kuweka maua, kuswali na kuwaombea waliouawa.

Kwa wengi ndani ya jamii hiyo, Amin Abdullah hakuwa tu mlinzi wa msikiti. Alikuwa mlinzi wa maisha.

ذو الحجة

HABARI
DAR ES SALAAM

MAHMOUD NYAMGUMA

# Mashinikizo dhidi ya Al-Aqsa yazua hofu mpya Jerusalem



Mvutano katika Msikiti wa Al-Aqsa mjini Jerusalem umeendelea kuongezeka huku mamlaka za Israel zikichukua hatua mpya kudhibiti na kubadilisha hadhi ya eneo hilo takatifu la Kiislamu.

Katika maendeleo ya karibuni, Israel imefuta vibali vya kuingia Jerusalem kwa wafanyakazi kadhaa wa Wakala wa Kiislamu wa Waqf wanaotoka Ukingo wa Magharibi, hatua ambayo itaathiri wafanyakazi wa muda mrefu wa Al-Aqsa akiwemo baadhi ya maimamu na viongozi wa dini.

Vyombo vya habari vya Palestina na Mashariki ya Kati vimeripoti kuwa hatua hizo zimekuja sambamba na kuongezeka kwa vizuizi kwa Waumini wa Kipalestina wanaotaka kuswali Al-Aqsa.

Kwa mujibu wa taarifa mbalimbali, zaidi ya wafanyakazi 30 wa Waqf wamewekewa marufuku au kuzuiwa kuingia katika eneo la msikiti huo katika miezi ya karibuni, huku baadhi wakikamatwa au kuhojiwa na vikosi vya usalama vya Israel.

Wapalestina wanaona hatua hizo kama jaribio la kudhoofisha mamlaka ya Waqf ya Jordan inayosimamia Al-Aqsa na kubadilisha mfumo wa kihistoria uliokuwepo kwa miongo mingi kuhusu usimamizi wa eneo hilo.

Mapema mwaka huu, Israel ilifunga Al-Aqsa kwa muda wa takribani siku 40 wakati wa mfungo wa Ramadhan na Sikukuu ya Eid, jambo lililotajwa kuwa la kwanza kutokea kwa kiwango hicho tangu mwaka 1967. Maelfu ya Wapalestina walilazimika kuswali nje ya milango ya mji wa kale wa Jerusalem baada ya kuzuiwa kuingia ndani ya msikiti huo.

Wachambuzi wa eneo hilo wanaonya kuwa Al-Aqsa inaendelea kuwa moja ya maeneo nyeti zaidi katika mgogoro wa Israel na Palestina, ambapo hatua yoyote dhidi ya msikiti huo huibua hasira kubwa katika ulimwengu wa Kiislamu.

ذُو الحِجَّةِ

HABARI

DAR ES SALAAM

NA MWANDISHI WETU

# Bima ya Kiislamu yakua nchini lakini bado ni 0.3% tu ya soko



## Uelewa bado chini

Sekta ya bima ya Kiislamu maarufu kama Takaful imeendelea kuonyesha dalili za ukuaji nchini Tanzania, huku Ripoti ya Utendaji wa Soko la Bima ya mwaka 2024 ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (Tira) ikionesha ongezeko la shughuli katika eneo hilo la huduma za kifedha zinazofuata misingi ya Shariah.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, madai katika sekta ya Takaful yaliongezeka hadi Sh96.5 milioni mwaka 2024 kutoka takribani Sh8 milioni mwaka 2023, jambo linaloonyesha ukuaji wa taratibu wa sehemu hiyo ya soko la bima nchini.

Ripoti hiyo pia inaonyesha kuwa kiwango cha jumla cha michango ya bima (Gross Written Premiums - GWP) katika Takaful kiliongezeka kutoka takribani Sh541 milioni mwaka 2023 hadi zaidi ya Sh4.6 bilioni mwaka 2024, hali inayoonyesha kupanuka kwa shughuli za bima zinazofuata misingi ya Shariah nchini.

Ripoti hiyo inaonyesha kuwa licha ya Takaful kubaki sehemu ndogo ya soko la bima nchini kwa asilimia 0.3 pekee, sekta hiyo ilikua kwa kasi kubwa kutoka Sh541 milioni mwaka 2023 hadi zaidi ya Sh4.6 bilioni mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 754.7

Ukuaji huo umeendelea kuonekana wakati sekta nyingine za bima nazo zikiendelea kupanuka mwaka 2024.

Katika soko la bima za kawaida (General Insurance Market), kiwango cha jumla cha michango ya bima (Gross Written Premiums — GWP) kiliongezeka kwa asilimia 21.3 kutoka Sh789.2 bilioni mwaka 2023 hadi Sh957.2 bilioni mwaka 2024.

Hata hivyo, Takaful bado ni sehemu ndogo ikilinganishwa na soko kubwa la bima za kawaida, hali inayoonyesha kuwa huduma hiyo bado ipo katika hatua za mwanzo lakini ikiwa na nafasi kubwa ya kukua zaidi siku zijazo.

Tofauti na bima za kawaida zinazotegemea mfumo wa kuhamisha hatari na uwekezaji wenye riba, Takaful hutegemea mfumo wa kusaidiana katika kugawana hatari kwa kuzingatia sheria za Kiislamu zinazokataza riba, kamari na gharar (kutokuwa na uhakika mkubwa katika miamala).

Gazeti la The Citizen, likinukuu ripoti ya Tira, lilieleza kuwa ongezeko hilo limechangiwa na waendeshaji kama First United Takaful na Zanzibar Insurance Corporation pamoja na kuingia kwa kampuni mpya kama Alibarakah Takaful Insurance.

Gazeti hilo pia lilinukuu sehemu ya ripoti ya Tira ikisema kuwa: "Kuongezeka kwa ushindani kumepanua upatikanaji wa bidhaa na kuongeza mwonekano wa bidhaa za bima zinazozingatia Sharia sokoni."

Hata hivyo, mshauri wa Takaful, Sheikh Yasser Awadh, alinukuliwa na The Citizen akisema kuwa sekta hiyo bado ina nafasi kubwa ya kukua licha ya kuendelea kukabiliwa na changamoto ya uelewa mdogo wa umma pamoja na uwekezaji hafifu.

Alibainisha kuwa wateja wengi watarajiwa bado hawaelewi kikamilifu namna Takaful inavyofanya kazi, hali inayozuia huduma hizo kupenya zaidi nje ya maeneo ya mijini na jamii zilizo tayari ndani ya mfumo rasmi wa bima.

Ripoti ya Tira inaonyesha kuwa sekta ya bima nchini iliendelea kunufaika na mageuzi mbalimbali ikiwemo matumizi ya teknolojia, ubunifu wa bidhaa pamoja na kuimarika kwa mifumo ya usambazaji wa huduma za bima.

Aidha, ripoti hiyo inaeleza kuwa sekta ya bima imeendelea kuwa na mchango katika juhudi za ujumuishaji wa kifedha na maendeleo ya uchumi wa taifa.

Pamoja na mwenendo huo mzuri, changamoto ya uelewa mdogo wa wananchi kuhusu huduma za bima bado inaonekana kuwa moja ya vikwazo vikubwa kwa ukuaji wa sekta hiyo, hususan katika huduma za Takaful ambazo bado ni mpya kwa sehemu kubwa ya wananchi.

Changamoto hiyo inaendana pia na hali ya sekta nzima ya bima nchini ambapo kiwango cha matumizi ya bima bado ni kidogo ukilinganisha na ukubwa wa idadi ya wananchi.

Hata hivyo, wadau mbalimbali wa sekta ya fedha wanaeleza kuwa ukuaji wa huduma za kifedha zinazofuata misingi ya Shariah unaweza kusaidia kuongeza matumizi ya Takaful nchini katika miaka ijayo.




UKHTI FATIMA SS

# Urusi kupanua huduma benki za Kiislamu

Urusi imetangaza mpango wa kupanua huduma za benki za Kiislamu huku mahitaji ya huduma za kifedha zinazofuata sheria za Kiislamu yakiendelea kuongezeka nchini humo.

Kwa mujibu wa benki kubwa ya Sber, mfumo huo wa majaribio ulianza mwaka 2023 katika maeneo manne yenye idadi kubwa ya Waislamu, yakiwemo Jamhuri ya Tatarstan, na baadaye ukaongezwa hadi mwaka 2028.

Mfumo wa fedha za Kiislamu unakataza riba na miamala ya kubahatisha, badala yake ukitegemea ushirikiano wa faida, ukodishaji na ufadhili unaounganishwa na mali halisi.

Akizungumza katika mkutano wa "Urusi na Ulimwengu wa Kiislamu" uliofanyika Kazan, Makamu Mkuu wa Sber, Oleg Ganeev, alisema mahitaji makubwa yapo katika huduma za kila siku kama akaunti, malipo, kadi na uwekezaji wa Kiislamu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Masoko ya Fedha ya Bunge la Urusi, Anatoly Aksakov, amesema nchi hiyo inaweza kupata viwango rasmi vya kwanza vya benki za Kiislamu ndani ya mwezi mmoja.

Maafisa wa Urusi pia wameeleza kuwa wanataka kutumia zaidi fedha za Kiislamu kuvutia uwekezaji kutoka nchi za Kiislamu na masoko ya kimataifa.



## Huduma Fedha za Kiislamu Uingereza zazidi kukubalika kwa wasio Waislamu

**Huduma za fedha za Kiislamu nchini Uingereza zinaendelea kupata umaarufu mkubwa kwa wasio Waislamu wanaotafuta mifumo ya kifedha inayozingatia maadili.**

**Kwa mujibu wa ripoti ya Benki ya Gatehouse iliyochapishwa na kituo cha Islam Channel, asilimia 88 ya Waislamu nchini Uingereza wako tayari kutumia taasisi za fedha za Kiislamu, huku karibu theluthi moja ya wasiokuwa Waislamu wakionesha utayari huo pia.**

**Mtendaji Mkuu wa Gatehouse Bank, Charles Haresnape, amesema ukuaji huo unatokana na uhusiano mkubwa uliopo kati ya misingi ya fedha za Kiislamu na uwekezaji wa kimaadili.**

**Amesema watu wengi sasa wanatafuta huduma za kifedha zinazozingatia uwazi, matumizi yenye maadili na uwekezaji usiohusisha shughuli zinazodhuru jamii.**

**Uingereza imeendelea kuwa moja ya nchi za Magharibi zilizo mbele katika sekta hiyo tangu ilipokuwa taifa la kwanza nje ya ulimwengu wa Kiislamu kutoa hati fungani za Kiislamu mwaka 2014.**

## Nigeria katika mkakati wa kufaidika soko la bidhaa za Halal

**Nigeria imechukua hatua mpya ya kujiimarisha katika uchumi wa kimataifa wa bidhaa za Halal unaokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya dola trilioni 7 duniani.**

**Hatua hiyo imeanza baada ya Waziri wa Nchi anayeshughulikia Bajeti na Mipango ya Uchumi, Dkt. Doris Nkiruka Uzoka-Anite, kuongoza kikao cha kwanza cha mpango wa kitaifa wa kuimarisha viwango vya Halal nchini humo.**

**Kwa mujibu wa TG News Nigeria, mkakati huo unalenga kuboresha uthibitishaji wa bidhaa za Halal, kuoanisha viwango vya Nigeria na viwango vya kimataifa pamoja na kuanzisha mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa bidhaa za Halal.**

**Dkt. Uzoka-Anite amesema hatua hizo zitasaidia kuongeza ushindani wa bidhaa za Nigeria katika masoko ya kimataifa.**

**Mpango huo unatarajiwa kuongeza fursa za mauzo ya nje hasa katika sekta za kilimo, usindikaji wa chakula, dawa na vipodozi.**

**Maafisa wa Nigeria wanaamini kuwa uchumi wa Halal unaweza kusaidia kuongeza ajira, kuvutia uwekezaji wa kigeni na kupanua vyanzo vya mapato ya nchi kupitia soko linalokuwa kwa kasi duniani.**

UKHTI FATIMA SS

# Somalia yazindua mpango wa fedha za Kiislamu kwa sekta ya mifugo

Serikali ya Somalia imezindua mpango mpya wa fedha za Kiislamu unaolenga kusaidia wafugaji, wafanyabiashara wa mifugo na biashara ndogo kupata huduma za kifedha zinazofuata sheria za Kiislamu.

Mpango huo unaojulikana kama Kobciye ulizinduliwa mjini Mogadishu Mei 23, 2026 katika hafla iliyohudhuriwa na maafisa wa serikali, taasisi za fedha, washirika wa maendeleo na sekta binafsi.

Kwa mujibu wa waandaaji, mpango huo utatoa huduma za kifedha kwa wafugaji, wasafirishaji wa mifugo, wafanyabiashara na wamiliki wa biashara ndogo zinazohusiana na uzalishaji wa mifugo.

Waandaaji wamesema mpango huo pia unalenga kuongeza upatikanaji wa fedha kwa wanawake, vijana na jamii ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikikosa huduma rasmi za kifedha.

Maafisa wa programu hiyo wamesema hatua hiyo itasaidia kukuza biashara, kuboresha upatikanaji wa masoko na kuongeza ushirikishwaji wa kifedha katika moja ya sekta muhimu zaidi za uchumi wa Somalia.

Kwa mujibu wa tovuti ya Dawan Africa, zaidi ya wafugaji na wafanyabiashara 1,000 wanatarajiwa kunufaika na mpango huo, huku watu 57 wakiwa tayari wamepata ufadhili kabla ya uzinduzi rasmi wa programu hiyo.

# Uganda yaomboleza kifo cha Sheikh aliyehubiri amani kwa baiskeli



Uganda imeingia katika majonzi kufuatia kifo cha Sheikh Abdul Lubega Bibowu, kiongozi wa dini aliyefahamika kwa safari zake za kila siku za baiskeli akiwa amebeba ujumbe wa amani, umoja na kuishi kwa kuvumiliana kati ya dini tofauti.

Sheikh Lubega alizikwa Alhamisi katika Hospitali ya Rufaa ya Taifa ya Kibuli mjini Kampala, huku viongozi wa dini, wananchi na wafuasi wake wakimkumbuka kama mtu aliyekuwa daraja la maelewano katika jamii.

Kwa miaka mingi, Sheikh huyo alikuwa akionekana akiendesha baiskeli kutoka Bunga kwenda Kampala huku akipeperusha leso nyeupe kama ishara ya amani na mshikamano. Wengi walimfahamu si tu kama Sheikh, bali kama mshauri, mpatanishi na mtu aliyekuwa tayari kuzungumza na kila mtu bila kujali dini, kabila au hadhi ya kijamii.

Waliofanya kazi naye wanasema alikuwa mnyenyekevu, mwenye upendo na aliyejitolea kuhimiza mazungumzo na kuvumiliana katika jamii.

Jamii ya Kiislamu baadaye ilitambua mchango wake kwa kumpatia eneo la kuishi karibu na msikiti aliokuwa akihudumia.

Kwa mujibu wa taarifa za awali, Sheikh Lubega alikuwa pia maarufu kwa uwezo wake wa kusimulia hadithi na kuwaleta pamoja watu kutoka makundi mbalimbali ya kijamii. Viongozi mbalimbali waliozungumza baada ya kifo chake wamesema urithi wake utaendelea kuhamasisha vizazi vijavyo kuhusu umuhimu wa amani, huruma na mshikamano wa kijamii.

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# Muongozo wa kupanga matumizi ya fedha kwa ajili ya Eid

**Eid ni moja ya nyakati zenye furaha kubwa kwa familia nyingi za Kitanzania. Ni kipindi cha ibada, shukrani, kuwatembelea ndugu, kusaidiana na kuwafurahisha watoto. Lakini pamoja na furaha hiyo, kwa baadhi ya familia Eid pia huambatana na mzigo mkubwa wa kifedha.**

**Nguo mpya, maandalizi ya chakula, safari za kwenda mikoani, fedha za Eid kwa watoto, michango ya kifamilia na kusaidia wenye uhitaji vinaweza kuongeza matumizi kwa kiwango kikubwa ndani ya muda mfupi.**

**Tatizo ni kwamba watu wengi huingia katika matumizi hayo bila maandalizi ya kutosha. Wengine hukopa, kutumia akiba yote au kutumia mshahara karibu wote katika siku chache za sherehe. Matokeo yake, baada ya**

Wataalamu wa fedha binafsi wanasema moja ya makosa makubwa ni kutenganisha kabisa masuala ya fedha na maadili ya Eid. Wakati Eid inafundisha shukrani, uwiano na kuwajali wengine, baadhi ya watu hujikuta wakifanya matumizi ya mashindano au ya kutaka kuonekana mbele ya jamii.

Kwa msingi huo, kupanga matumizi mapema ni muhimu.

Hatua ya kwanza ni kuweka bajeti halisi kabla ya Eid kufika. Familia inapaswa kujiuliza mapema: tutatumia kiasi gani kwa chakula, mavazi, usafiri, zawadi na fedha za watoto? Kuwa na kiwango maalumu cha matumizi hakupunguzi furaha ya Eid. Kinyume chake, husaidia familia kusherehekea kwa utulivu bila kuingia katika madeni yasiyo ya lazima.

Pia wataalamu wanashauri watu kuepuka matumizi yanayofanywa kwa presha za kijamii. Sio lazima kila familia ifanye Eid kwa kiwango sawa. Wengine hujikuta wakinunua vitu kwa sababu ya kuona majirani, ndugu au mitandao ya kijamii.

Lakini ukweli ni kwamba Eid yenye amani ya akili huwa bora kuliko Eid ya matumizi makubwa yanayoacha msongo wa mawazo baadaye.

Katika jamii ya Kitanzania, Eid pia ni kipindi muhimu cha kusaidia wengine. Hata hivyo, wataalamu wa fedha wanasema kusaidia hakumaanishi kuharibu kabisa hali yako ya kifedha. Ukarimu mzuri unatakiwa kwenda sambamba na mipango mizuri.

Baadhi ya wataalamu wanashauri familia kuanza kuweka akiba ya Eid miezi kadhaa kabla ya sikukuu badala ya kusubiri wiki za mwisho. Hata kiasi kidogo kinachowekwa kila mwezi kinaweza kupunguza mzigo mkubwa wa ghafla.

Baada ya Eid, ni muhimu pia kufanya tathmini ya matumizi yaliyofanyika. Je, fedha nyingi zilitumika wapi? Ni matumizi gani yalikuwa ya lazima na yapi yangeweza kupunguzwa? Tathmini hiyo inaweza kusaidia familia kupanga vizuri zaidi Eid inayofuata.

Wataalamu wa fedha wanaeleza kuwa afya nzuri ya kifedha haimaanishi kutotumia fedha katika sherehe, bali kutumia kwa uwiano unaolinda maisha ya baada ya sherehe pia.

Mwisho wa siku, lengo la Eid si mashindano ya matumizi, bali ni ibada, mshikamano, shukrani na furaha ya pamoja. Na zawadi kubwa zaidi kwa familia si matumizi ya gharama kubwa, bali ni kusherehekea kwa utulivu, upendo na mipango mizuri ya kifedha.





# Anzia sokoni: Kuanzia uchambuzi wa mteja hadi kubuni bidhaa

**Watu wengi wanaotaka kuanzisha biashara huamini kuwa mafanikio huanza kwa kupata wazo la kipekee. Ndiyo maana baadhi yao hukaa kwa muda mrefu wakitafuta "wazo kubwa" wakiamini kuwa ubunifu pekee ndio msingi wa biashara yenye mafanikio.**

**Lakini wataalamu wa biashara changa (startups) wanaeleza kuwa bidhaa nyingi zilizofanikiwa duniani hazikuanza kwa ubunifu wa ajabu sana. Zilianza kwa kuelewa maisha ya watu, changamoto zao na mambo yanayowasumbua kila siku. Kwa maneno mengine, biashara nyingi imara huanza kwa kumwelewa mteja kabla ya kujenga bidhaa.**

## Hatua ya kwanza: Kumjua mteja vizuri

Kabla ya kufikiria programu, bidhaa, huduma au teknolojia, mwanzilishi anatakiwa kuelewa mteja wake ni nani. Anafanya kazi gani? Anaishi maisha gani? Ni changamoto gani humsumbua mara kwa mara? Tatizo hilo hutokea katika mazingira gani?

Hatua hii ni muhimu kwa sababu huwezi kujenga suluhisho zuri ikiwa humwelewi mtu unayetaka kumsaidia. Biashara nyingi hufeli kwa sababu hujaribu kuhudumia "kila mtu." Lakini ukweli ni kwamba startups nyingi zenye mafanikio huanza kwa kutatua tatizo la kundi maalumu sana la watu.

Kadri mwanzilishi anavyomwelewa mteja wake vizuri, ndivyo anavyoweza kuona matatizo ambayo wengine hawaoni.

## Hatua ya pili: Kugundua maumivu ya mteja

Baada ya kumjua mteja, hatua inayofuata ni kutafuta kile kinachomsumbua kweli. Katika biashara za kisasa, hili huitwa "maumivu ya mteja" (customer pain). Haya ni matatizo yanayopoteza muda, fedha, nguvu au yanayowalazimisha watu kutumia njia ngumu zisizo na ufanisi.

Kwa mfano, ikiwa wafanyabiashara wanatumia muda mwingi kufuatilia taarifa kwa mikono, wagonjwa wanakaa foleni ndefu kupata huduma rahisi, au watu wanahangaika kufanya kazi ambayo ingeweza kurahisishwa, hapo kuna nafasi ya biashara.

Tatizo linapokuwa kubwa na la kujirudia mara kwa mara, thamani ya suluhisho huongezeka. Wataalamu wa biashara wanaonya kuwa baadhi ya waanzilishi hupenda sana suluhisho lao kabla hawajathibitisha kama tatizo lenyewe ni muhimu vya kutosha kwa watu.

Ndiyo maana hatua ya kuelewa "maumivu" ni muhimu kabla ya kuendelea mbele.

## Hatua ya tatu: Kuangalia kama watu wako tayari kulipa

Baada ya kugundua tatizo, mwanzilishi anatakiwa kujiuliza swali muhimu: Je, watu wako tayari kulipia suluhisho hili? Hii ndiyo hatua inayotenganisha wazo la kawaida na biashara halisi.

Kuna matatizo ambayo watu hulalamikia sana lakini hawapo tayari kutoa fedha kuyatatua. Lakini pia kuna matatizo ambayo watu wako tayari kulipia haraka kwa sababu yanawagharimu muda, pesa au usumbufu mkubwa.

Wataalamu wa biashara wanasema ishara nzuri huwa pale ambapo watu tayari wanatumia fedha kutafuta njia mbadala, hata kama suluhisho lililopo si bora sana. Kwa mfano, ikiwa kampuni tayari zinatumia fedha nyingi kufanya kazi fulani kwa njia ya zamani au isiyo na ufanisi, startup inayorahisisha kazi hiyo inaweza kuwa na nafasi kubwa sokoni.

Hapa ndipo mwanzilishi anapoanza kuona kama tatizo lina thamani ya kibiashara au ni malalamiko ya kawaida tu.

## Hatua ya nne: Kupima kama biashara inaweza kujiendesha

Kuthibitisha kuwa watu wako tayari kulipa bado hakutoshi. Hatua inayofuata ni kuangalia kama biashara yenyewe inaweza kujiendesha kifedha. Hapa ndipo suala la "uchumi wa biashara" (business economics) linaingia.

Mwanzilishi anatakiwa kufikiria kwa kina: Itagharimu kiasi gani kutengeneza bidhaa? Itagharimu kiasi gani kupata mteja mmoja? Bei ya huduma itakuwa kiasi gani? Je, mapato yanaweza kuzidi gharama? Biashara inaweza kuwa na wateja wengi lakini bado ikafa ikiwa gharama zake ni kubwa kuliko mapato yake.

Ni kwa sababu hii wawekezaji wengi hawaangalii ubunifu pekee; wanaangalia kama biashara inaweza kuendelea kuishi kifedha kwa muda mrefu. Wataalamu wa biashara wanaonya kuwa kosa kubwa la baadhi ya waanzilishi ni kujenga bidhaa kwanza halafu baadaye waanze kufikiria namna ya kupata faida.

## Hatua ya mwisho: Kujenga bidhaa baada ya kuthibitisha

Ni baada ya kupitia hatua zote hizo ndipo sasa mwanzilishi anatakiwa kuanza kujenga bidhaa au huduma yake. Katika hatua hii, tayari anakuwa amemwelewa mteja, amegundua tatizo lake, amethibitisha kuwa watu wako tayari kulipia suluhisho na ameona kuwa biashara inaweza kujiendesha. Hii hupunguza hatari ya kujenga bidhaa ambayo hakuna anayehitaji.

Wataalamu wa startup wanashauri kuanza na bidhaa ndogo inayoweza kujaribiwa mapema badala ya kutumia miaka mingi kujenga mfumo mkubwa usio na uhakika wa kupokelewa sokoni.

Maoni ya watumiaji wa mwanzo huwasaidia waanzilishi kuboresha bidhaa zao hatua kwa hatua.

Katika ulimwengu wa biashara za kisasa, mafanikio hayategemei sana kuwa na wazo la ajabu kuliko kila mtu mwingine. Mara nyingi hutegemea uwezo wa kuelewa watu vizuri zaidi kuliko washindani wako.




# Mlipuko mpya wa Ebola: Tutahadhari bila kutaharuki

Mlipuko mpya wa Ebola katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Uganda umeibua tahadhari kubwa ya kiafya, baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuutangaza kuwa Dharura ya Kimataifa ya Afya ya Umma.

Mlipuko huu unasababishwa na virusi vya Bundibugyo, aina ya Ebola ambayo kwa sasa haina chanjo wala tiba maalumu iliyoidhinishwa. Hata hivyo, WHO inasisitiza kuwa Ebola ni ugonjwa hatari lakini unaoweza kudhibitiwa kwa kugundua wagonjwa mapema, kuwatenga, kuwahudumia na kufuatilia watu waliokutana nao.

Kwa mujibu wa WHO, hadi Mei 16, 2026, DRC ilikuwa imeripoti wagonjwa wanane waliothibitishwa maabara, wagonjwa 246 wanaoshukiwa na vifo 80 vinavyoshukiwa katika jimbo la Ituri. Uganda iliripoti wagonjwa wawili waliothibitishwa Kampala, mmoja akiwa amefariki, wote wakihusishwa na safari kutoka DRC.

Taarifa za baadaye zimeripoti kuongezeka kwa wasiwasi, huku WHO ikieleza kuwa idadi halisi inaweza kuwa kubwa kuliko inayothibitishwa sasa. DW imeripoti WHO ikitaja karibu wagonjwa 750 wanaoshukiwa na vifo 177 vinavyoshukiwa, huku hatari ndani ya DRC ikiwekwa katika kiwango cha "juu sana."

Kinachoongeza hofu si Ebola pekee, bali mazingira ya mlipuko. Ituri na maeneo jirani yana mwingiliano mkubwa wa watu, changamoto za usalama, vituo vya afya vyenye rasilimali chache na harakati za mipakani. Hali hizi zinaweza kufanya ugonjwa kusambaa haraka ikiwa ufuatiliaji hautaimarishwa.

Profesa Mohamed Yakub Janabi, Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, amesema hatua muhimu sasa ni kutambua wagonjwa mapema, kufuatilia waliokutana nao, kulinda wahudumu wa afya na kushirikisha jamii. Amesisitiza kuwa chanjo si silaha pekee; huduma za haraka kama kurejesha maji mwilini, oksijeni na uangalizi maalumu zinaweza kuokoa maisha.

Kwa wananchi, ujumbe mkuu ni tahadhari bila taharuki. Ebola huambukizwa kupitia kugusa damu au majimaji ya mwili wa mgonjwa au aliyefariki kwa Ebola. Dalili zinazopaswa kuripotiwa haraka ni homa kali, uchovu mkubwa, kutapika, kuharisha, maumivu ya mwili na dalili za kutokwa damu.

Nchi jirani zinapaswa kuimarisha ufuatiliaji mipakani, mawasiliano kwa jamii na utayari wa vituo vya afya. Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania pia umetoa tahadhari kwa raia wake kufuatilia taarifa rasmi kuhusu mlipuko huo.

Somo kubwa ni hili: Ebola hushindwa mapema, si kwa hofu, bali kwa uwazi, taarifa sahihi, huduma za haraka na ushirikiano wa jamii.



SHEIKH Shaaban Mussa 0786 272 323

# Toba na kujirekebisha, safari endelevu baada ya Ramadhan

**Miongoni mwa mafundisho makubwa sana ya Ramadhan ni kumfanya Muislamu arejee kwa Mwenyezi Mungu kwa toba ya kweli na kujitathmini nafsi yake. Mwezi huo mtukufu ni kipindi cha rehema, msamaha, na urejeo wa mja kwa Mola wake Mlezi baada ya kujitwika makosa na uzembe katika maisha yake ya kila siku.**

## Toba ni nini?

Toba ni kurejea kwa Mwenyezi Mungu kwa kuacha dhambi, kujuta kwa dhati juu ya yaliyopita, na kuwa na azma ya kutorudia tena maasi hayo.

Pia ni mchakato wa ndani wa moyo unaoambatana na matendo ya mabadiliko ya kweli.

Ndani ya Ramadhan, milango ya rehema huwa wazi zaidi, na Waislamu hujikuta wakiomba msamaha kwa wingi, wakilia mbele ya Mola wao Mlezi, na wakijitahidi kuacha maovu yao. Hii ni ishara kwamba nafsi ya mwanadamu ina uwezo wa kubadilika ikiwa itaelekezwa vizuri.

Lakini swali muhimu ni hili: je, toba hii inaendelea baada ya Ramadhan?

## Toba ya kweli na namna ya kuidumisha

Kwa baadhi ya watu, Ramadhan huleta mabadiliko ya muda mfupi tu, lakini baada ya mwezi huo kuisha, hurudi tena katika makosa yao ya zamani. Hii ni dalili ya wazi ya toba isiyo thabiti au isiyokidhi vigezo na masharti.

Toba ya kweli si ya msimu, bali ni safari endelevu ya maisha. Muislamu anapaswa kuwa katika hali ya toba kila siku, kwa sababu binadamu hakosi makosa. Tofauti ni kwamba Muumini wa kweli huyaacha makosa yake na kumrudia Mwenyezi Mungu mara kwa mara.



Miongoni mwa njia muhimu za kudumisha toba baada ya Ramadhan ni kujitathmini nafsi kila siku (muhasaba). Muislamu anapaswa kujiuliza: leo nimefanya nini kizuri? Nimekosea wapi? Na nitarekebisha vipi kesho yangu?

Pia, kuomba msamaha mara kwa mara (istighfar) ni sehemu muhimu ya safari ya toba. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alikuwa akiomba msamaha mara nyingi kila siku, jambo linaloonesha umuhimu wa tabia hii katika maisha ya Muislamu.

Aidha, ni muhimu kuepuka mazingira yote yanayomrudisha mtu katika maasi. Toba haiwezi kudumu ikiwa mtu anaendelea kujihusisha na vyanzo vya dhambi. Hivyo basi, mabadiliko ya kweli yanahitaji pia mabadiliko ya mazingira na tabia.

Kujenga marafiki wema na kushiriki katika vikao vya elimu ya dini pia husaidia sana kuimarisha toba. Mazingira mazuri humkumbusha mtu kumcha Mwenyezi Mungu na kumtia moyo kuendelea katika njia sahihi.

Toba pia inahitaji unyenyekevu wa moyo. Muislamu anapaswa kutambua kuwa bila rehema za Mwenyezi Mungu hawezi kufanikiwa. Hii humfanya aendelee kumtegemea Allah katika kila hatua ya maisha yake.

## Milango ya kurejea iko wazi muda wote

Kwa hakika, anayefanikiwa si yule asiyeanguka dhambini kabisa, bali ni yule anayerejea haraka kwa Mwenyezi Mungu kila anapokosea. Huo ndio uzuri wa Uislamu, milango ya kurejea iko wazi muda wote.

Hivyo basi, baada ya Ramadhan, kila Muislamu anapaswa kuendeleza roho ya toba na kujirekebisha kila siku, bila kusubiri mwezi maalum au tukio maalum.

Lakini pamoja na toba na kujirekebisha nafsi, kuna somo la mwisho na muhimu sana katika mfululizo huu wa Ramadhan, nalo ni uhusiano wa muda mrefu na Allah kupitia ibada endelevu.

Katika makala inayofuata na ya mwisho ya mfululizo huu, tutazungumzia kuhusu Uhusiano Endelevu na Allah – Lengo Kuu Baada ya Ramadhani, na jinsi ya kuifanya Ramadhani iwe mwanzo wa maisha mapya ya karibu na Mola Mlezi.

Eid Al-Adha

MAKALA MAALUM

Na Said Rajab
0783 650 803

# Eid al-Adh'ha - kielelezo cha imani, utii na kujitoa kwa Allah

**Sikukuu ya Eid al-Adh'ha hufuatia baada ya siku tukufu ya Arafa, ambayo ni moja ya siku muhimu za Hijja. Miongoni mwa dhana na ujumbe mkuu wa Hijja ni kujisalimisha na kuwa mtiifu kwa Allah 'Azza Wajallah'.**
**Tunaposoma visa vya kusisimua kuhusu Nabii Ibrahim, Nabii Ismail na Hajar (amani ya Allah iwashukie wote), tunashuhudia mfano wa kipekee wa utii na kujisalimisha mbele ya Allah, jambo ambalo ndilo hasa maana ya Uislamu. Kwa hakika, kujisalimisha kwa Allah ndiyo maana halisi ya neno 'Islam'. Hivyo, maana na kiini cha Uislamu imejikita katika ibada ya Hijja, inayotukumbusha dhamira na malengo yetu katika maisha.**

## Eid al-Adh'ha ni alama ya utii

Katika siku hii tunaadhimisha vitendo vya utii na kujisalimisha vilivyofanywa na Nabii Ibrahim na familia yake, wakati alipoamrishwa kumpeleka Hajar pamoja na mwanawe Ismail katika jangwa lisilokuwa na watu na kuwaacha huko peke yao.

Nabii Ibrahim alijisalimisha kwa Allah na kutii amri yake. Hajar alipotambua kilichokuwa kinaendelea, alilia kwa sauti kubwa: "Ee Ibrahim! Unatuacha katika bonde hili ambalo hakuna watu wanaoishi?" Alirudia swali hilo bila kupata jibu, ndipo akamuuliza: "Allah amekuamrisha kufanya hivi?"

Nabii Ibrahim akajibu: "Ndiyo."

Hajar (amani ya Allah imshukie) akasema: "Basi Allah hatatuacha tuangamie." Hivyo naye akajisalimisha kwa Allah. Aidha, Ismail alipokuwa mkubwa, Ibrahim (amani ya Allah imshukie) alipokea amri kutoka kwa Mola wake ya kumtoa sadaka mwanawe. Alisalimu amri hiyo ya Mwenyezi Mungu, na mwanawe pia akafanya hivyo.

Familia ya Ibrahim ilikuwa ni familia ya utii na kujisalimisha mbele ya Allah 'Azza Wajallah'. Walipitia mitihani na majaribu mbalimbali kutoka kwa Mwenyezi Mungu, lakini matokeo yake kila mara yalikuwa ni utii na kujisalimisha.

Sikukuu zote mbili, Eid al-Adh'ha na Eid al-Fitr, huja baada ya kutekelezwa kwa nguzo ya Uislamu, ikiwa ni kitendo cha utii. Kwa hiyo, Eid al-Adh'ha na Eid al-Fitr ni ukumbusho wa kila mwaka kwamba maisha haya ni mtihani na tunapaswa kuwa watiifu iwapo tunataka kufanikiwa.

Mara moja kila mwaka, Waislamu kutoka kila kona ya dunia, wenye hadhi na tamaduni tofauti hukumbushwa ujumbe mmoja: "Jisalimishe kwa Allah, kuwa mtiifu kwa Allah." Je, tunasikia ujumbe huu?

Kama Nabii Ibrahim alivyopewa mitihani katika maisha yake yote ili kuona kama atasalimu amri au la, nasi pia tutapewa mitihani ili kuona kama tutatii amri za Mwenyezi Mungu au tutakataa. Ni muhimu kutambua kwamba mahangaiko, harakati na magumu yote huambatana na jitihada za kuwa watiifu.

Lakini tukimtii Allah 'Azza Wajallah' tutakuwa miongoni mwa watu wema kama Nabii Ibrahim na familia yake Peponi, kama Allah anavyosema: "Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wako pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na MasEidiqi, na Mashahidi, na watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!" [Qur'an, 4:69].

Eid pia inabeba ujumbe mwingi maridhawa, ambao miongoni mwao ni maelezo ya wazi ya ushahidi wa imani kwamba "Muhammad ni Mjumbe wa Allah", jambo linalomaanisha kumfuata Mtume Muhammad katika maamrisho yake, kuacha yale aliyokataza, kuamini yote aliyotuambia na kumuabudu Mwenyezi Mungu kama alivyoelekeza.

Allah anasema: "Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume. Na mkigeuka, basi yaliyo juu yake ni aliyobebeshwa, na yaliyo juu yenu ni mliyobebeshwa nyinyi. Na mkimtii yeye mtaongoka. Na hapana juu ya Mtume ila kufikisha ujumbe waziwazi." [Qur'an, 24:54].

Kimsingi, kama kweli unatamani kuingia Peponi, basi unachotakiwa kufanya ni kuwa mtiifu, kwani Mtume amemuhakikishia Pepo yeyote atakayemfuata: "Umma wangu wote wataingia Peponi isipokuwa wale watakaokataa."

Sahaba mmoja akauliza: "Nani atakayekataa?" Mtume akajibu: "Yeyote anayenitii ataingia Peponi, na yeyote anayeniasi amekataa." [Bukhari].

Vilevile, Allah 'Azza Wajallah' anatuonya katika Qur'an kuhusu matokeo ya kumuasi. Anasema: "Na anayemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha." [Qur'an, 4:14].

Miongoni mwa ujumbe mwingine wa Eid ni kwamba Waislamu wote ni wamoja na ndugu. Tunakusanyika pamoja kwa sala na kushirikiana katika baraka za Eid. Katika nyakati hizi, tunapaswa kujitahidi kuimarisha udugu wetu na kurekebisha tofauti zetu kwa kuzingatia ukweli. Vijana wa Kiislamu, tumieni fursa ya Eid kuwa wema kwa wazazi wenu, na tambueni ya kwamba utii kwa wazazi ni utii kwa Allah 'Azza Wajallah', alimradi tu hauhusishi kumuasi Mwenyezi Mungu.

Kaeni mbali na pombe, sigara na dawa za kulevya, kwa kuwa vitu hivyo huharibu moyo, akili na jamii. Sisi Waislamu tunapaswa kuimarisha utii wetu na kujisalimisha kwa Allah, kwa kuwa muda tulionao ni mchache sana.

Tukumbuke kwamba wale tulioswali nao Eid mwaka jana, baadhi yao sasa ni wakazi wa makaburini. Nasi siku moja tutaungana nao.

Tusidanganywe na maisha ya duniani ambayo furaha yake haidumu. Kifo huharibu furaha ya watu, hivyo tutafute furaha ambayo ndani yake hakuna kifo.

Tuichukulie dunia hii kama mahali pa kufanya kazi kuelekea Akhera, kama Allah 'Azza Wajallah' anavyosema kuhusu kutafuta Pepo: "Na anayeitaka Akhera, na akazifanyia juhudi amali zake, naye ni muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni yenye kukubaliwa." [Qur'an, 17:19].

Eid Al-Adha

فتاوى



SHEIKH
Shaaban Mussa
0786 272 323

# Yajuzu kufunga Arafa ilhali mtu ana deni la Ramadhan?

**Swali: Ni ipi hukumu ya kufunga siku ya tisa ya Dhul-hija?**

**Jibu:** Siku ya tisa ya Dhul-hijjah ni Siku ya Arafah. Kufunga siku hiyo ni sunna kwa watu wote. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) aliulizwa kuhusu kufunga Siku hiyo ya Arafah, akasema: "Mwenyezi Mungu hufuta kwa kufunga siku hiyo dhambi za mwaka uliopita na mwaka unaofuata."

Kwa hiyo, inapendekezwa kufunga Siku ya Arafah kwa wanaume na wanawake, isipokuwa kwa aliye katika Hijja. Huyo hafungi siku ya Arafah akiwa hija mwaka huo. Ama wasiokuwa mahujaji, sunna kwao ni kufunga ikiwa wanaweza. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Ni ipi fadhila ya anayefunga Siku ya Arafah?**

**Jibu:** Mwenye kufunga Siku ya Arafah hupata ujira mkubwa. Imethibiti kutoka kwa Mtume (Allah amshushie rehema na amani) kuwa amesema: "Mwenyezi Mungu hufuta kwa kufunga Siku ya Arafah dhambi za mwaka uliopita na mwaka unaofuata." Yaani kwa sharti ya kujiepusha na dhambi kubwa kama zilivyoeleza hadith nyingine. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi.

**Swali: Je, inajuzu kufunga Siku ya Arafa ilhali mtu ana siku za kulipa za Ramadhan?**

**Jibu:** Hujaji hafungi Siku ya Arafah kwa sababu Mtume (Allah amshushie rehema na amani) alisimama Arafah hali ya kuwa amefungua, na alikataza kufunga huko. Ama wasiokuwa mahujaji, inapendekezwa kwao kufunga kwa sababu ni siku yenye fadhila kubwa. Kufunga kwake hufuta dhambi za mwaka uliopita na mwaka unaofuata, na ndani yake kuna kheri nyingi.

Kama tulivyodokeza, ambaye si hujaji, imependekezwa kufunga lakini ikiwa ana saumu za kulipa (qadhaa) basi aanze kwanza kuzilipa. Na akifunga Siku ya Arafah na siku tisa za mwanzo za Dhul-Hijjah kwa nia ya qadhaa, basi hilo ni jambo jema. Na Allah ndiye Mjuzi zaidi

**Swali: Je, kufunga Arafah kunafuta dhambi kubwa?**

**Jibu:** Kwa mujibu wa maana ya dhahiri ya Sunna, kufunga huko kunafuta dhambi ndogo. Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Swala tano, Ijumaa hadi Ijumaa, na Ramadhan hadi Ramadhan ni kafara ya dhambi ziliyo kati yake ikiwa dhambi kubwa zimeepukwa." Na Swala ni kubwa zaidi kuliko Hijja.

Pia Mtume (Allah amshushie rehema na amani) amesema: "Hija iliyokubaliwa haina malipo isipokuwa Pepo." Na akasema: "Atakayehiji bila kufanya uchafu wala maasi, atarudi akiwa safi kama siku aliyozaliwa na mama yake." Pia amesema: "Hakuna siku ambayo Mwenyezi Mungu huwaachia watu wengi zaidi kutoka Motoni kuliko Siku ya Arafah."

Kwa hiyo, inatarajiwa kwa wafungaji kuachwa huru na Moto na kusamehewa. Lakini maana ya wazi ya hadith ni kwamba Hijja, kama ibada nyingine, hufuta dhambi ndogo isipokuwa kama mtu ametubia dhambi kubwa. Ndiyo maana amesema: "Atakayehiji bila kufanya uchafu wala maasi..." Yaani aliyekwenda kwa Mola wake bila kuendelea kushikilia dhambi, Hijja yake huwa ni kafara ya makosa yake. Na Allah nsiye Mjuzi zaidi.



ذُو الحِجَّة

# NASAHA ZA WIKI

0787 503 085

NA YUSUFU AMINI



# Kamari, adui anayeangamiza jamii kimyakimya



Michezo ya kamari imekuwa mtindo mpya wa maisha kwa watu wengi hapa nchini na duniani kwa ujumla. Utitiri wa matangazo, yakiwamo ya televisheni na idhaa za redio yanayohamasisha kucheza kamari, kupatikana kirahisi kwa simu za mkononi, pamoja na kamari kutambuliwa kisheria kama mchezo halali unaochangia pato la taifa, vimechangia kwa kiasi kikubwa michezo hiyo kushamiri.

Ukipita kwenye mitaa ya jiji la Dar es Salaam, utaona kila baada ya mita 20 hadi 30 kuna mashine za kubeti jambo ambalo linachangia vijana wengi kucheza kamari.

Imebainika kuwa baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari na vyuo vikuu wanaingia darasani huku wakiwaza mafanikio ya haraka na hivyo kujiingiza kwenye michezo ya kamari kama njia ya mkato ya kujiingizia kipato. Hali hii imekuwa ikiongeza utegemezi na kupunguza bidii ya kazi na elimu.

Ukweli usio na shaka ni kwamba kampuni za kamari ndizo zinazonufaika zaidi, huku wachezaji wengi wakiishia kupoteza fedha, muda na hata heshima zao.

Mara nyingi ushindi mdogo wa awali huwavuta wachezaji wengi wa kamari katika mtego wa kuendelea kucheza. Kadiri mtu anavyozidi kucheza, ndivyo tamaa na utegemezi vinavyoongezeka.

Shetani hutumia tamaa ya utajiri wa haraka kuwashawishi watu kuingia katika michezo hii, ambayo mara nyingi huacha maumivu na majuto makubwa. Watu wanaweza kushinda kiasi kidogo cha fedha mwanzoni na kudhani kuwa wameanza safari ya mafanikio. Hatimaye hujikuta wameishiwa fedha na wengine huuza mali zao, hukopa bila uwezo wa kulipa, na hata kuiba ili waendelee kucheza kamari.

Madhara haya huenea hadi kwenye familia, ambapo uhusiano wa kifamilia huvunjika kutokana na kushindwa kutimiza majukumu ya msingi. Baadhi ya watu hupoteza ajira kwa sababu ya kutumia muda mwingi kufuatilia matokeo ya kamari badala ya kufanya kazi kwa bidii.

Vijana, ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa, wanapoingia katika uraibu huu uchumi wa nchi pia huathirika kwa kupungua uzalishaji na kuongezeka kwa utegemezi wa kiuchumi. Ingawa kuna maoni mengi na tofauti kuhusu michezo ya kamari, ukweli ni kwamba kamari inaathiri vijana wengi, ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa na wakiwa pia ni asilimia 52 ya Watanzania wote.

## Mwenyezi Mungu amekataza kamari

Kucheza kamari ni dhambi, na pia ni kosa la jinai, na ndiyo maana hata nchi zilizoendelea, kwa kuelewa madhara ya kamari, kuna maeneo maalumu ya michezo hiyo tofauti na Tanzania ambako kamari inachezwa hadharani, vijijini mpaka mijini.

Licha ya michezo ya kubahatisha kuchangia kuongezeka kwa pato la taifa, ukweli unabaki kuwa, kamari ina madhara kijamii, kiuchumi na hata kiafya kwa mtu mmoja mmoja. Mara nyingi tumekuwa tukishuhudia vijana wakipoteza muda na pesa kwenye michezo ya kamari, hali inayosababisha kupata msongo wa mawazo na wakati mwingine hata kujiua kutokana na hasara kubwa wanazopata.

Kwa upande wa madhara ya kijamii, uraibu wa kamari unatajwa kuchangia kuongezeka kwa vitendo vya uhalifu, kwani imebainika kuwa baadhi ya vijana wasioweza kumudu gharama za kucheza hujikuta wakijihusisha na vitendo vya wizi na uporaji ili kupata pesa za kucheza kamari.

Kutokana na madhara hayo, ndiyo maana Mwenyezi Mungu ameharamisha kamari. Hilo lipo wazi ndani ya Qur'an pale Mwenyezi Mungu aliposema: "Enyi mliyoamini! Bila ya shaka ulevi, na kamari, na kuabudu masanamu, na kupiga ramli, ni uchafu katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufanikiwa." [Qur'an, 5:90].

Kwa kuzingatia maonyo ya aya hii, maoni ya wananchi, tafiti na hali halisi ya ongezeko la vijana wanaojihusisha na kamari, nadhani ipo haja kwa serikali na jamii nzima ya Watanzania kuona ukubwa wa tatizo la kamari na madhara yake ili kunusuru kizazi chetu dhidi ya mtego huu wa shetani.

Serikali, taasisi za dini pamoja na mashirika ya kijamii yana dhima kubwa ya kutoa elimu kuhusu madhara ya kamari katika ngazi zote za elimu, na kupitia kampeni za kitaifa.

Aidha, kuwepo kwa kanuni kali za kudhibiti matangazo ya kamari ni jambo la msingi ili kupunguza ushawishi wake, hususan kwa vijana. Wazazi nao wana wajibu wa kufuatilia mienendo ya vijana wao na kuwasaidia kuelewa thamani ya kazi na uvumilivu badala ya kutafuta utajiri wa haraka.

MAKALA MAALUM

SHEIKH Seif Ruga
0712 690 811



# Ukweli kuhusu dua na masharti yake

**Dua ni ibada na ni moja ya sababu muhimu za mafanikio ya mja hapa duniani na kesho Akhera. Hata hivyo, athari za dua hazipimwi kwa kupatikana kile kinachoombwa mara moja, kwani wakati mwingine mwombaji hujibiwa kwa kucheleweshewa alichoomba au kuondoshewa balaa.**
**Wakati mwingine jibu la dua huchelewa kutokana na maasi, kukosa subira au moyo kughafilika. Uislamu umebainisha kuwa kujibiwa kwa dua hakufungamani na matamshi pekee, bali kunahitaji unyenyekevu wa kweli, kuhudhurisha moyo, kuwa na haja ya dhati ya kinachoombwa, kufuata Sunna za Mtume pamoja na kumuomba Allah Mtukufu kupitia majina yake matukufu.**

## Dua ni silaha ya Muumini

Dua ni miongoni mwa tiba zenye manufaa makubwa, kwani huondosha balaa, huizuia au kuipunguza hata baada ya kuteremshwa. Waumini wanapaswa kumtegemea Allah Mtukufu, kumuomba na kumwelekea Yeye katika mambo yao yote.

Ibn Taymiyyah (Allah amrehemu) amesema: "Dua ni miongoni mwa sababu alizozikadiria Allah Mtukufu. Kutegemea sababu pekee bila kumtegemea Allah ni kufanya ushirikina katika tauhidi; na kupuuza sababu kabisa ni upungufu wa akili; na kuziacha kabisa ni kasoro katika sharia. Mja anatakiwa kumtegemea Allah Mtukufu katika dua na matamanio yake, na Allah humpa anachotaka."

Kwa upande wake, Imam Ibn Qayyim (Allah amrehemu) amesema: "Mwenye kuelewa vizuri suala hili (la kuchukua sababu) atanufaika sana. Hatategemea kudura ya Allah pekee kwa ujinga au uzembe, bali atapambana na kudura kwa kudura na kuzuia kudura kwa kudura."

Maana yake ni kwamba, mambo yote ya dunia na Akhera yanategemea sababu na matendo. Kilicho muhimu ni mtu kufanya juhudi na kuomba kwa dua zilizothibiti, kwani dua ni miongoni mwa ibada bora zaidi. Allah ametukataza kuvuka mipaka katika kuomba, na ametusisitiza kumuomba Yeye pekee kwa kufuata mafundisho ya Mtume wake kama ilivyo katika ibada nyingine.

## Hali za dua

Mtume wa Allah amesema: "Hakuna Muislamu anayeomba dua isiyokuwa na uovu wala kukata undugu ndani yake isipokuwa Allah atampa kwa dua hiyo mambo matatu. Ima atamjibu dua yake haraka, au atamwekea akiba Akhera, au atamuepushia shari kwa kiwango kile kile alichoomba." Masahaba wakasema: "Basi tuzidishe kuomba..."

Katika hadith nyingine, Mtume wa Allah amesema: "Hakuna kinachoongeza umri isipokuwa wema, na hakuna kinachorudisha qadar isipokuwa dua; na mtu hunyimwa riziki kwa sababu ya madhambi anayofanya."



Kutokana na maelezo hayo, Imam Ibn Qayyim amefafanua hali za dua na mabalaa kwa kusema: "Dua ina hali tatu: Kwanza, iwe na nguvu kuliko balaa, hivyo huiondoa. Pili, iwe dhaifu kuliko balaa, hivyo balaa humshinda mja lakini dua hupunguza athari zake. Tatu, dua na balaa vilingane, hivyo kila kimoja humzuia mwenzake."

Maneno haya yanaonesha umuhimu wa dua na kwamba muumini hupata kheri katika hali zote. Mtume (rehema na amani zimshukie) alisema: "Dua ni ibada," kisha akasoma aya isemayo: "Na Mola wenu amesema: Niombeni, nitakujibuni..." [Qur'an 40:60].

Hakuna mja anayemuelekea Allah kwa dua isipokuwa humpa moja ya mambo matatu. Huenda akamjibu dua yake haraka, akampa thawabu Akhera, au akamuepushia shari hata kama hakumpa kile alichokiomba duniani, kwa hekima anayojua Yeye.

## Vizuizi vya dua

Miongoni mwa vizuizi vikubwa vya kujibiwa dua ni kuwa na haraka ya kujibiwa na kukosa subira. Mara nyingi mtu huomba dua, lakini anapoona jibu limechelewa huchoka na kusema: "Nimeomba sana lakini sijajibiwa," kisha huacha kuomba.

Imam Ibn Taymiyyah amesema: "Mja hujibiwa maadamu hafanyi haraka..." Kauli hii inaonesha kuwa mafanikio katika jambo lolote yanafungamana na subira, na kwamba faraja huja pamoja na dhiki." Ibn Qayyim ameifananisha hali hiyo na mtu aliyepanda mbegu kisha akaacha kuitunza kwa sababu ameona imechelewa kuchipua.

Kizuizi kingine cha kujibiwa dua ni kuomba mambo yasiyopendwa na Allah Mtukufu, kama kuomba maovu au mambo ya dhambi, kuwa na imani dhaifu, kufanya maasi pamoja na kula haramu.

Katika hadith iliyosimuliwa na Abu Huraira (Allah amridhie), Mtume (rehema na amani zimshukie) amesema: "Muombeni Allah hali ya kuwa mna yakini ya kujibiwa, na jueni kuwa Allah hakubali dua ya mtu ambaye moyo wake umeghafilika." [Tirmidhi na Hakim].




MAKALA MAALUM

Na Junaynat Ally Dama
0789 201 383

# Misingi minne ya mafanikioya kimkakati

Katika dunia ya leo yenye ushindani mkubwa, kufanya kazi kwa juhudi pekee haitoshi tena. Taasisi, biashara na hata watu binafsi wanahitaji uwezo wa kufikiri na kutenda kimkakati (strategically) ili kufikia mafanikio ya muda mrefu.

Wataalamu wa uongozi na biashara wanaeleza kuwa mafanikio mengi ya kudumu hujengwa juu ya misingi minne muhimu: fikra za kimkakati, mwelekeo wa kimkakati, mipango ya kimkakati na utekelezaji wa kimkakati.

## Fikra za kimkakati (Strategic thinking)

Msingi wa kwanza ni uwezo wa kufikiri zaidi ya matatizo ya muda mfupi.

Watu wenye fikra za kimkakati hawaangalii tu kilicho mbele yao leo, bali pia matokeo ya baadaye ya maamuzi wanayofanya sasa. Wao hujiuliza: "Je, tunafikiria kwa upana wa kutosha?"

Wataalamu wanasema fikra za kimkakati zinahitaji uwezo wa kubadilika kulingana na mazingira, kusikiliza mitazamo tofauti na kuhoji mazoea au imani ambazo watu wengi huzichukulia kama ukweli wa kawaida.

Katika biashara, viongozi wasiofikiri kimkakati mara nyingi hushughulikia "moto wa kila siku" bila kujiandaa kwa mabadiliko ya soko, teknolojia au tabia za wateja.

Kwa mtu binafsi pia, maisha yasiyo na fikra za kimkakati yanaweza kujaa maamuzi ya haraka yasiyo na dira ya muda mrefu.

## Mwelekeo wa kimkakati (Strategic direction)

Baada ya kuwa na fikra pana, hatua inayofuata ni kujua nini hasa ni muhimu.

Changamoto kubwa ya dunia ya sasa si ukosefu wa fursa pekee, bali wingi wa kelele, taarifa na mambo ya kufanya. Ndiyo maana watu na taasisi nyingi hujikuta zikiwa na shughuli nyingi lakini maendeleo kidogo.

Mwelekeo wa kimkakati unahusu kuchagua mambo muhimu zaidi na kuacha mengine.

Hii inahitaji kufanya maamuzi magumu na wakati mwingine kukubali kuwa huwezi kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Wataalamu wa biashara husema kuwa mkakati mzuri si tu kujua nini cha kufanya, bali pia kujua nini usifanye.

Katika timu au taasisi, mwelekeo wa pamoja huwasaidia watu kufanya kazi kwa lengo moja badala ya kila mtu kwenda kivyake.

## Mipango ya kimkakati (Strategic planning)

Ndoto au maono pekee havitoshi bila mpango wa utekelezaji.

Mipango ya kimkakati inahusu kuvunja malengo makubwa katika hatua ndogo zinazoeleweka. Hapa ndipo watu huamua kazi itafanyikaje, ni nani atafanya nini na ni mfumo gani utatumika. Wataalamu wanaeleza kuwa taasisi nyingi hushindwa si kwa sababu ya kukosa maono, bali kwa sababu ya kukosa mifumo mizuri ya kazi.

Mipango mizuri huweka sheria za kazi, ratiba, vipaumbele na njia za kupima maendeleo. Pia huwasaidia watu kupunguza mkanganyiko na matumizi mabaya ya muda na rasilimali.

Kwa mtu binafsi, mipango ya kimkakati inaweza kujumuisha kuweka ratiba za fedha, masomo, biashara au maendeleo binafsi badala ya kuishi kwa maamuzi ya kubahatisha kila siku.

## Utekelezaji wa kimkakati (Strategic execution)

Msingi wa mwisho na muhimu zaidi ni utekelezaji. Watu wengi wana mawazo mazuri na mipango mizuri, lakini wachache wana nidhamu ya kutekeleza kwa mwendelezo. Wataalamu wanasema mafanikio makubwa mara nyingi hutokana si na motisha ya muda mfupi, bali tabia zinazojirudia kila siku.

Utekelezaji wa kimkakati unahusisha mawasiliano ya wazi, kujenga utaratibu wa kazi unaoeleweka na kuimarisha viwango vinavyotarajiwa.

Katika taasisi, viongozi wanapaswa kuwa mfano wa tabia wanazotaka kuona kwa wengine. Katika maisha binafsi pia, mafanikio hujengwa zaidi na tabia za kila siku kuliko malengo yanayoandikwa mwanzoni mwa mwaka halafu kusahaulika.

Mwisho wa siku, mkakati si karatasi ya mipango wala maneno ya motivasheni pekee. Ni uwezo wa kufikiri kwa upana, kuchagua muhimu, kupanga kwa umakini na kutekeleza kwa nidhamu kila siku.

"Afya"is natural source of sweet drinking water from underground stream which is blended with essential minerals to support and aid perfect metabolism.




WATERCOM LIMITED
P.o. Box 20409, Plot N.4005, Kisarawe11 area Temeke, Dar es Salaam, Tanzania. www.watercomtz.com, Email:info@watercomtz.com

NA UKHTI FATIMA SS
0789 201 383

# Uongozi wa kweli ni mzigo ambao watu wengi huuona kama heshima

**Watu wengi huangalia uongozi kwa mtazamo mwepesi na finyu. Kuongoza mikutano. Kutoa maamuzi. Kuwa na majibu ya kila swali. Kuonekana mwenye nguvu kuliko wengine.**
**Lakini wataalamu wanasema uongozi wa kweli si sauti kubwa wala uwezo wa kutoa amri. Ni mambo mengi, tata na mengine kinzani. Uwezo wa kubeba presha bila kuwaumiza watu walioko chini yako, kusimamia hisia, mkanganyiko, migogoro na matarajio ya watu wengi kwa wakati mmoja - haya yote yanakuja na uongozi.**
**Wengi hupenda nafasi ya uongozi, lakini wachache huelewa na kuvumilia uzito wake. Tuone baadhi ya mambo yanayoashiria uzito wa uongozi.**

## Kusimamia hisia kabla ya kusimamia watu

Katika mazingira ya kazi, timu humuangalia kiongozi wao kama kipimo cha hali ilivyo.

Kiongozi anayejazbika kirahisi, anayelipuka kwa hasira hueneza hofu lakini anayebaki mtulivu wakati wa presha huwafanya watu wajisikie salama hata katikati ya changamoto.

Wataalamu wa uongozi wanaeleza kuwa watu hawafuati tu maamuzi ya viongozi; wanafuata pia hali zao za kihisia na ndiyo maana uwezo wa kusimamia hisia zako umekuwa sehemu muhimu ya uongozi wa kisasa.

## Kusikiliza kuliko kuongea

Watu wengi hudhani viongozi bora ni wanaoongea sana. Lakini taasisi nyingi zilizofanikiwa zimejengwa na viongozi wanaojua kusikiliza. Kusikiliza kabla ya kutenda huwasaidia viongozi kuelewa kile kinachosemwa na kile kisichosemwa.

Maswali mazuri huwa na nguvu kuliko majibu ya haraka. Kiongozi anayesikiliza hujenga mazingira ambayo watu wanaweza kutoa mawazo yao bila kuogopa kubezwa au kuadhibiwa. Hapo ndipo ubunifu na uaminifu huanza kukua.

## Uwazi katikati ya mkanganyiko

Katika nyakati ngumu, watu hutafuta uwazi kuliko ukamilifu na ndiyo maana kazi ya kiongozi si kuwa na majibu yote, bali kusaidia watu kuelewa mwelekeo.

Kiongozi bora hueleza "kwa nini" kabla ya "fanyeni." Huweka wazi malengo, vipaumbele na sababu za maamuzi. Wataalamu wa mawasiliano ya taasisi wanaeleza kuwa timu nyingi hazivunjwi na ukosefu wa uwezo, bali ukosefu wa uwazi.

Watu wanapokosa mwelekeo, hofu hujazana kwenye nafasi iliyoachwa na ukimya.

## Maamuzi magumu katika taarifa zisizo kamili

Katika maisha halisi, viongozi wengi hawapewi taarifa zote kabla ya kufanya maamuzi. Wanalazimika kuamua katikati ya shinikizo, muda mchache na kutokuwa na uhakika ndiyo maana uongozi si sanaa ya kuwa mkamilifu. Ni sanaa ya kubeba uzito wa uchaguzi.

Wakati mwingine kiongozi hulazimika kufanya mazungumzo magumu, kukemea utendaji mbovu au kuwawajibisha watu ambao hawatimizi wajibu wao. Kuepuka maamuzi hayo kwa sababu ya kutaka kupendwa huweza kuharibu taasisi nzima.

## Huruma bila kupoteza viwango

Uongozi wenye afya si ukali wa kudumu wala upole usio na mipaka. Kiongozi bora hujua kusawazisha matokeo na ustawi wa watu. Anajali afya ya kihisia ya timu yake, lakini pia haachi viwango vya kazi vishuke.

Wataalamu wa saikolojia ya kazi wanaeleza kuwa watu hufanya vizuri zaidi wanapohisi kuthaminiwa, kusikilizwa na kuwa salama kutoa mawazo au makosa yao bila kudhalilishwa. Hiyo ndiyo tofauti kati ya kuongoza kwa hofu na kuongoza kwa imani.

## Kujenga watu, si kutengeneza wafuasi

Katika mifumo ya zamani, viongozi wengi walitaka kuwa kitovu cha kila kitu. Lakini viongozi bora wa leo hujenga watu wanaoweza kusimama wenyewe. Hujua lini waongoze mbele na lini warudi nyuma ili wengine wakue. Huongoza kwa mafunzo, motisha na mfano, si kwa amri pekee.

Watu wengi hawahitaji kusukumwa kila siku; wanahitaji kuona maana ya kile wanachokifanya na ndiyo maana viongozi bora huamsha ari, si utii wa nje tu.

## Kukubali makosa

Moja ya vipimo vigumu zaidi vya uongozi ni uwezo wa kusema: "Nilikosea." Viongozi wanaojifanya hawakosei hujenga utamaduni wa hofu na kuficha makosa. Lakini wanaokubali udhaifu wao hujenga kuaminika. Unyenyekevu huwa na nguvu kubwa kuliko ukamilifu wa kujifanya.

Mwisho wa siku, uongozi si cheo. Si ukubwa wa ofisi. Si sauti kali mezani. Ni uwezo wa kubeba watu bila kuwavunja. Kuwapa mwelekeo bila kuwaondolea utu wao. Kuwafanya wawe bora zaidi kuliko walivyokuwa jana. Na hapo ndipo uongozi wa kweli huanza — si katika mamlaka, bali katika namna mtu anavyowagusa na kuwaongoza wengine.

MAKALA MAALUM SEHEMU YA 2

Na Said Rajab
0783 650 803



# Waislamu walivyopoteza dira yao!

**Katika sehemu ya kwanza ya makala haya wiki iliyopita, tulibainisha juhudi za Khalifa Nur ad-Din Mahmud pamoja na kamanda wake wa kijeshi, Salahuddin Al-Ayubi katika kurejesha dhana ya dola kama chombo cha msingi cha kubeba ujumbe wa Kiislamu duniani.**

**Leo tumalizie sehemu ya mwisho kwa kuangazia harakati za utawala wa Uthmaniyyah (Ottoman), ambao katika siku zao za mwanzo uliunganisha ardhi za Waislamu zilizokuwa zimetawanyika na kuasisi upya dola ya Kiislamu.**

Moja ya nyakati muhimu katika historia ya sasa ya ulimwengu ilikuwa ni kufutwa kwa dola ya Kiislamu ya Ottoman, au Ukhalifa wa Ottoman mwaka 1924.

Hapa, siyo tu kwamba mamlaka ya kisiasa yalianguka, bali pia taasisi iliyowakilisha umoja wa kisiasa wa Waislamu, licha ya udhaifu wake, ilisambaratika kabisa.

Tangu wakati huo, hakukuwa tena na dola moja ya Waislamu iliyokuwa ikichukua nafasi ya nyingine katika utawala, bali dhana moja ilichukua nafasi ya nyingine.

Dola ndogo ndogo zenye mrengo wa kikabila na kitaifa zilichukua nafasi ya dola moja kubwa ya Kiislamu iliyoungana na kuwajumuisha wote, yaani taifa la Waislamu duniani.

Siku hizi, mipaka bandia ya kitaifa inayowazuia Waislamu kuungana tena na kuwa taifa moja ndiyo inayotukuzwa zaidi. Utiifu umehama kutoka kwenye aqida ya Kiislamu na kuelekezwa kwenye uzalendo wa nchi pamoja na utaifa unaoundwa na mipaka ya kijiografia.

Tawala nyingi zilizoibuka baadaye katika ardhi za Waislamu hazikujengwa juu ya msingi kwamba sharia ya Mwenyezi Mungu ndiyo inayopaswa kuongoza dola, bali zilijengwa juu ya katiba za kisekula zinazopata uhalali wake kutoka kwenye sheria ya kimataifa.

Kwa hiyo, umma wa Kiislamu ulibadilika kutoka mfumo wa kisiasa unaotegemea utekelezaji wa sharia za Mwenyezi Mungu, hata kama ulikuwa na dosari katika utekelezaji wake, hadi mifumo inayotenganisha dini na utawala, huku haki ya kutunga sheria ikipewa mabunge badala ya Mwenyezi Mungu.

Ningependa kusisitiza kile kilichothibitishwa awali, kwamba utekelezaji wenye dosari wa Uislamu hauwezi kulinganishwa na utekelezaji mzuri wa mfumo mwingine wowote, hata kama unatekelezwa vizuri kiasi gani. Utekelezaji wa Uislamu pekee ndio uadilifu, na utekelezaji wa mifumo mingine yoyote ni ukandamizaji.

Migogoro ya kiuchumi inayojirudia katika nchi za Waislamu, madeni makubwa, pamoja na mgawanyiko wa kisiasa si dalili za muda mfupi, bali ni matokeo ya muundo wa kifikra na kisiasa ambao haukutokana na aqida ya Waislamu.

Majadiliano kuhusu kuleta mageuzi ndani ya mfumo uliopo hayana maana, kwa sababu dosari ipo katika msingi, si katika matawi. Dola inapoongozwa kwa mtazamo wa kuhifadhi mfumo uliopo badala ya kutekeleza Uislamu, na wakati maslahi finyu ya kitaifa yanapopewa kipaumbele kuliko maslahi mapana ya umma, mkengeuko utaendelea hata kama sura na kaulimbiu zitabadilika.

Ningependa kuukumbusha umma kwamba Qur'an Tukufu ililetwa ili kuutawala umma, si kuwa chanzo cha baraka za kiroho pekee. Kujizatiti kwetu katika ibada ni kichocheo cha nidhamu na pia ni chachu ya ukombozi dhidi ya ushawishi wa matamanio na utiifu kwa mamlaka yoyote inayopingana na aqida yetu.

Kudurusu historia haina maana ya kuzingatia yaliyopita pekee, bali pia kuelewa mifumo ya kupanda na kushuka kwa mataifa. Dira ya kisiasa inapokengeuka kutoka katika sharia ya Mwenyezi Mungu, udhaifu hujilimbikiza, na inaporekebishwa, majeraha huanza kupona.

*Itaendelea wiki ijayo, Insha Allah.*

Na Junaynat Ally Dama



SEHEMU YA 3

# Jinsi akili bandia (AI) inavyo badilisha dunia

## Ajira zisizoathiriwa kirahisi na AI

Kadri mjadala kuhusu akili bandia unavyoendelea, simulizi moja imekuwa ikijirudia: kwamba mashine zitachukua nafasi ya binadamu katika kazi nyingi. Hata hivyo, uchambuzi wa kina unaonyesha picha iliyo changamano zaidi. Si kazi zote ziko hatarini kwa kiwango sawa. Kwa kweli, kuna aina ya kazi na ujuzi ambao, kwa sasa, bado unaonekana kuwa ngumu kwa AI kuiga kikamilifu.

Kwanza ni kazi zinazohitaji ubunifu wa hali ya juu. Ingawa mifumo ya AI inaweza kuandika, kuchora, au hata kutunga muziki, mara nyingi hufanya hivyo kwa kuiga mifumo iliyopo.

Ubunifu wa binadamu, kwa upande mwingine, hauishii katika kuchanganya yaliyopo; una uwezo wa kuvunja kanuni na kuanzisha mwelekeo mpya.

Hapa ndipo tofauti ya msingi ipo kati ya "kutengeneza kitu" na "kuanzisha kitu kipya." Kwa maana hiyo, sekta kama sanaa, uandishi wa ubunifu, ubunifu wa kibiashara, na uvumbuzi bado zinategemea sana uwezo wa kipekee wa binadamu.

## Kazi za akili ya kihisia

Pili ni kazi zinazohitaji akili ya kihisia (emotional intelligence). Hii ni uwezo wa kuelewa, kusoma na kujibu hisia za watu wengine kwa usahihi. Katika taaluma kama ualimu, ushauri nasaha, uongozi, na huduma za afya, mwingiliano wa kibinadamu si nyongeza—ndiyo msingi wa kazi yenyewe.

AI inaweza kutoa majibu sahihi kitaalamu, lakini mara nyingi hukosa muktadha wa kihisia unaohitajika katika maamuzi nyeti ya kibinadamu.

## Kazi za zinazohitaji maadili

Tatu ni kazi zinazohitaji maamuzi ya kimaadili na kijamii. Haya ni maeneo ambayo hata wataalamu wanakubaliana kuwa AI ina mipaka.

Mashine zinaweza kufuata kanuni, lakini hazina dhamira (moral agency). Haziwezi kuwajibika kwa maamuzi yao kwa maana ya kijamii na kisheria kama binadamu wanavyofanya.

Katika sekta kama sheria, uongozi wa umma, na utungaji sera, maamuzi hayawezi kutegemea data pekee; yanahitaji muktadha, thamani, na wakati mwingine huruma.

## Kazi za mazingira yasiyotabirika

Nne ni kazi zinazohitaji ustadi wa mikono katika mazingira yasiyotabirika. Ingawa roboti zimepiga hatua kubwa, bado zinapata changamoto katika mazingira yenye mabadiliko ya haraka au yasiyotabirika.

Mafundi, wahandisi wa matengenezo, wakulima katika mazingira halisi, na wataalamu wa huduma za dharura wanafanya kazi katika hali ambazo haziwezi kuwekewa kanuni rahisi za kompyuta. Hapa, uzoefu wa moja kwa moja na uwezo wa kubadilika papo hapo ni muhimu zaidi kuliko usahihi wa kiotomatiki.

## Kazi za muingiliano wa kijamii

Tano ni kazi zinazohusisha mwingiliano wa kijamii wa hali ya juu, kama uongozi na ushawishi.

Kuongoza timu, kujenga uaminifu, kushawishi watu, na kusimamia migogoro ni mambo yanayohitaji mchanganyiko wa mawasiliano, hisia, na uelewa wa kijamii.

Haya ni maeneo ambayo AI inaweza kusaidia, lakini haiwezi kuchukua nafasi ya binadamu kikamilifu.

## Tusiwe na uhakika sana

Hata hivyo, ni muhimu kutofikia hitimisho la haraka kwamba kazi hizi "ziko salama kabisa." Ukweli uliopo ni kwamba AI haitachukua nafasi ya kazi zote, lakini itabadilisha jinsi kazi hizo zinavyofanywa.

Mwalimu wa leo, kwa mfano, anaweza kutumia AI kuboresha maandalizi ya somo au tathmini ya wanafunzi. Daktari anaweza kutumia AI kusaidia uchunguzi wa awali. Kiongozi anaweza kutumia data inayotolewa na AI kufanya maamuzi bora zaidi. Hivyo, hata katika kazi zinazoonekana salama, mabadiliko hayakwepeki.

Kwa wataalamu wengi, ujumbe unaojitokeza ni mmoja: mustakabali si wa "binadamu dhidi ya mashine," bali ni wa "binadamu pamoja na mashine." Wale watakaoweza kutumia AI kama nyongeza ya uwezo wao watakuwa na

MUSSA IMANI SHEHA ZANZIBAR
0773 181 494

SEHEMU YA 9



# SIMULIZI YA MTUME MUSA (AMANI YA ALLAH IMSHUKIE)

## VISA VYA MITUME NA MASWAHABA

**Katika toleo lililopita, tuliona mjadala mkali wa kwanza baina ya Musa na Fir-aun, ambapo Mtume Musa alimsimamishia mpinzani wake hoja makini za kitauhidi, zenye lengo la kumtambulisha Allah Ta'ala na upweke wake katika uumbaji, uendeshaji viumbe na namna anavyostahiki kuabudiwa.**
**Tulianza kuona udhaifu wa Fir-aun kwa kushindwa kuzijibu hoja za Mtume Musa (Allah amshushie rehema na amani), na akaishia kutumia lugha za kejeli.**

### Miujiza ya Mtume Musa

Katika kikao kile, Fir-aun alitumia vitisho na kusema: " Kama utashikilia (kwamba kuna) mungu mwengine badala yangu kwa lazima nitakufanya miongoni mwa wenye kufungwa gerezani." [Qur'an, 26:29]

Mtume Musa akasema: "Ijapokuwa nitakuletea kitu (muujiza) kilicho wazi?" Akasema: "Ulete kama wewe miongoni mwa wasemao kweli."

Basi (Mtume Musa) akaitupa fimbo yake chini mara ikawa nyoka wa dhahiri. Na akatoa mkono wake mara ukawa mweupe (kweli kweli) kwa watazamao."

Fir-aun Akasema kuwaambia wakuu waliomzunguka: "Kwa hakika huyu ni mchawi ajuae sana. Anachotaka ni kukutoweni katika nchi yenu kwa uchawi wake, basi mnanishauri nini?"

Wakuu hao walikubaliana na jabari huyo, "Wakasema, 'Hakika huu ni uchawi wa wazi'" [Qur'an, 26:30-33].

### Mazingatio:

Mafunzo ya Mitume kuyahusisha na uchawi au wendawazimu, imekuwa ndiyo mtindo wa makafiri wa zama zote walipofikiwa na Mitume wao, kama tuonavyo madai ya makafiri wa leo eti Qur-an ni kitabu cha uganga (uchawi).

Mwenyezi Mungu anasema katika Surat Adhaariyaat: "Basi ndivyo hivi hivi hakuna Mtume yoyote aliyewajia wale wa kabla yao (hawa Makureishi) ila walisema: huyu ni mchawi au mwendawazimu. Je wameusiana (wameambizana) jambo hili? (la), bali wao ni watu waovu" [Qur'an, 51:52-53].

Katika sura nyengine, Qur'an inasimulia: "Wakasema, 'Hakika hawa wawli (Musa na Haruna) ni wachawi, wanataka kukutoweni katika ardhi yenu kwa uchawi wao na kuondoa sera (mila) iliyo bora kabisa." [Qur'an, 20:60].

"Wakasema, 'Umetujia ili utuondowe katika yale tuliyowakuta nayo baba zetu na ili ukubwa uwe wenu nyinyi (wawili tu) katika nchi (hii) sisi hatuwezi kukuaminini." [Qur'an,10:78].

### Fir-aun ajiita mungu hadharani

Qur'an inatusimulia kwamba, baada ya kufikiwa na wajumbe wa Mola wake na kumuonesha miujiza ya wazi, alipandwa na hasira na kibri kikamtawala.

Aliitisha mkutano na kuwaambia wananchi wake kwamba wasibabaike na kwamba yeye ndiye mungu, na waliokuja ni wachawi tu. Akasema kwa kusaidiana na wachawi hodari wa Misri, serikali yake itawashughulikia na kuwamaliza mara moja.

Qur'an inasema: "Je, zimekufikia habari za Musa? Alipoitwa na Mola wake kwenye Bonde Takatifu Tuwaa. (Mola wake akamwambia) nenda kwa Fir-aun hakika yeye amevuka mipaka. Umwambie, 'Je unapenda kujitakasa nami nitakuongoza kwa Mola wako ili umche?' Basi alimuonesha ishara (miujiza) mikubwa mikubwa. Lakini alikadhibisha na akaasi. Kisha alirudi nyuma akaanza (jitihada za kuwazuilia watu wasimfuate Musa). Basi aliwakusanya (watu) na akanadi akasema, 'Mimi ndiye mola wenu mkuu'" [Qur'an, 79 15-24].

"Na Fir-aun akasema, 'Enyi wakuu, simjui kwa ajili yenu mungu asiyekuwa mimi, basi ewe hamana (nifanyie matufali) uniwashie moto juu ya udongo (wa matufali hayo ili yakauke), unijengee mnara ili (nipande) nikamchungulie mungu wa Musa, na mimi namdhani yu katika waongo (hakuna mungu)'" [Qur'an, 28:38].

"Subhanallah!" huu ndio ukafiri. Na ndio madhara ya mtu kujisahau anapokuwa madarakani, yanayowafika wakuu na waheshimiwa wengi hadi leo! Nas-alullaahal-aafiya!

### Ushauri wa wakuu wa nchi kwa mfalme Fir-aun

Bila shaka, ujio wa Mitume hao na kumfikishia ujumbe kutoka kwa Mola wao ulimshughulisha sana Fir-aun, mawaziri, makuhani na wasaidizi wao, kwani kulitishia kupoteza nyadhifa, mamlaka na tawala yao dhalimu.

Kwa hiyo, walifikiria sana lipi la kufanya katika kumkabili Musa na aliyokuja nayo. Wakuu walimshauri Fir-aun kwamba, kwa vile alichokuja nacho Musa na ndugu yake ni uchawi, awakusanye wachawi wote walio katika mamlaka yake wakabiliane (washindani) na Musa (Allah amshushie rehema na amani) kwa njia hiyo hiyo.

Fir-aun alikubaliana na ushauri huo bila ya pingamizi kwani aliamini hakuna njia nyengine ya kuuhami ufalme wake ila kupata msaada wa wachawi na makuhani. Qur'an inasema: "Fir-aun akasema, 'Nileteeni kila mchawi hodari'" [Qur'an, 10:79]. Ama kweli "Mwisho wa ubaya ni fedheha" haya yatazidi kudhihiri hapo mbele!

Kabla ya kuona jinsi agizo la mfalme Fir-aun lilivyotekelezwa, turejee tena aya zifuatazo: "Na hakika tulimuonesha (Fir-aun) ishara zetu zote lakini alikadhibisha akakataa. Akasema, 'Umetujia kututoa katika nchi yetu kwa uchawi wako ewe Musa. Basi sisi tutakuletea uchawi mithili (kama) huo, basi fanya ahadi (ya mkutano) baina yetu na wewe.

***Itaendelea inshaAllah***

ذُو الحِجَّة

MAKALA YA AFYA

Na Junaynat Ally Dama

# Utafiti mpya: Kahawa yahusishwa na msongo wa mawazo

Watu wengi hutumia kahawa au vinywaji vyenye kafeini ili kuongeza nguvu, kuondoa usingizi au kusaidia akili kuwa makini zaidi. Lakini utafiti mpya uliowasilishwa Marekani umeibua mjadala mpya kuhusu uhusiano kati ya matumizi makubwa ya kafeini na dalili za msongo wa mawazo (depression).

Utafiti huo uliwasilishwa Mei 17, 2026 katika mkutano wa mwaka wa Chama cha Wataalamu wa Magonjwa ya Akili Marekani (American Psychiatric Association – APA) uliofanyika San Francisco, Marekani. Habari hizo ziliripotiwa na tovuti ya afya ya Medscape.

Watafiti kutoka Chuo cha Tiba cha Chuo Kikuu cha Arizona mjini Tucson walichunguza watu zaidi ya 1,000 wenye umri kati ya miaka 22 hadi 60 ili kuona uhusiano kati ya matumizi ya kafeini, usingizi, uchovu, msongo wa mawazo na afya ya akili.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, watu waliokuwa wakitumia kiasi kikubwa cha kafeini kila siku walionekana kuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa na dalili kali za msongo wa mawazo.

Mtafiti mkuu wa utafiti huo, Mira Kaur Marwah, amesema watafiti walitaka kuelewa kama watu hutumia kafeini kama njia ya kupambana na dalili za uchovu, kukosa nguvu au kushuka kwa hali ya kihisia bila kutambua athari zinazoweza kujitokeza baadaye.

Utafiti huo uligundua kuwa watu waliokuwa wakinywa vikombe vitatu hadi vinne vya vinywaji vyenye kafeini kwa siku, pamoja na wale waliotumia zaidi ya hapo, walikuwa na alama za juu zaidi katika vipimo vya dalili za msongo wa mawazo.

Aidha, watafiti walibaini kuwa matatizo ya usingizi, uchovu, msongo wa mawazo na usingizi wa mchana vilikuwa vinaenda sambamba na ongezeko la dalili za afya duni ya akili.

Hata hivyo, watafiti pia waliona jambo lililowashangaza. Kwa baadhi ya washiriki waliokuwa na matatizo makubwa ya usingizi, matumizi ya kafeini yalionekana kupunguza kwa kiasi fulani ukali wa uhusiano kati ya kukosa usingizi na msongo wa mawazo.

Wataalamu wa afya ya akili wanasema matokeo hayo yanaonyesha kuwa suala la kafeini na afya ya akili ni tata zaidi kuliko watu wengi wanavyodhani.

Daktari Gregory Scott Brown, profesa mshiriki wa tiba katika Chuo cha Tiba cha Chuo Kikuu cha Houston, Texas, ambaye hakushiriki katika utafiti huo, amesema utafiti huo ni wa muhimu lakini bado unaibua maswali mengi zaidi.

Ameeleza kuwa kafeini huathiri watu tofauti kwa namna tofauti, hivyo si sahihi kutoa hitimisho la jumla kuwa kila mtu anayekunywa kahawa nyingi atapata msongo wa mawazo.

Pia wataalamu wameonya kuwa utafiti huo haukuchunguza tofauti kati ya kahawa nyeusi, kahawa yenye sukari nyingi au aina nyingine za vinywaji vyenye kafeini. Aidha, utafiti huo haukuhusisha vinywaji vya soda.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, matumizi ya kiasi cha wastani cha kahawa kwa watu wengi huwa salama. Tatizo linaweza kuanza pale matumizi yanapokuwa makubwa kupita kiasi au pale mtu anapotegemea kafeini kila siku ili kupambana na uchovu, msongo au kukosa usingizi.

Wataalamu wanashauri watu wanaopata matatizo ya usingizi, mapigo ya moyo kwenda kasi, wasiwasi wa mara kwa mara au mabadiliko ya kihisia kuangalia pia kiwango cha kafeini wanachotumia kila siku.

Ingawa utafiti zaidi bado unahitajika, ujumbe mkubwa kutoka kwa watafiti ni kwamba afya ya akili haiathiriwi na jambo moja pekee. Usingizi, msongo wa mawazo, uchovu na tabia za kila siku kama matumizi ya kafeini vinaweza kuwa na uhusiano mkubwa kuliko watu wengi wanavyofikiria.



NA ZAHARANI BARAKA

Eid Al-Adha

MATUKIO YENYE MAZINGATIO

# Miiko, wajibu na Sunna katika sherehe za Eid

**Kutoka kwa mama Aisha (Allah amridhie yeye na baba yake) amesimulia kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) aliingia nyumbani kwake huku wasichana wawili wadogo wakiimba mashairi kuhusu vita vya Bu'ath. Mtume akalala na kugeuza uso wake. Mara Abubakr (Allah amridhie) akaingia, na alipowaona wale wasichana wawili akamkemea Aisha akisema: "Mazumari ya kishetani mbele ya Mjumbe wa Allah?" akikusudia nyimbo hizo. Mtume akamwambia: "Waache." Katika riwaya nyingine, Mtume alisema: "Ewe Abubakr, kila watu wana sikukuu yao, na hii Eid ni sikukuu yetu." [Bukhari na Muslim].**

**Riwaya nyingine ya Ahmad bin Hanbal inaeleza kuwa Mtume (rehema na amani zimshukie) alisema: "Ili Mayahudi wajue kwamba katika dini yetu kuna wasaa na wepesi. Hakika nimetumwa kwa dini iliyo nyepesi na ya wastani (ya kati na kati)." *[Bukhari]***

## Mafundisho ya tukio

Eid mbili ni alama kubwa za dini ya Kiislamu na ni miongoni mwa ibada tukufu. Nafsi za watu zimeumbwa kupenda furaha, ndiyo maana Mtume (rehema na amani zimshukie) amehalalisha sikukuu mbili kubwa – Eid al–Fitri na Eid al–Adh'ha.

Imepokewa hadith kutoka kwa Anas bin Malik (Allah amridhie) kwamba, Mtume (rehema na amani zimshukie) alipofika Madina aliwakuta watu wakiwa na siku mbili za kucheza na kujifurahisha, akasema: "Hakika Allah amewabadilishia siku mbili zilizo bora kuliko hizo; siku ya Fitri na siku ya Adh'ha." [Abu Daudi].

Siku za Eid ni siku zinazobeba furaha na shangwe katika nafsi za watu, huku zikijaza nyoyo bishara na faraja

## Eid katika zama za Mtume

Katika zama za Mtume wa Allah (rehema na amani zimshukie), Eid ilikuwa ni ibada, furaha, kuonesha neema za Allah, kuunganisha familia na jamii, pamoja na kuingiza furaha kwa watoto, jamaa na marafiki.

Mtume alikuwa mpole na mwenye kuwafurahisha wakeze, lakini furaha hiyo iliambatana na mipaka ya maadili na sharia za Kiislamu, si kufanya maasi au kuacha kumtii Allah. Wanazuoni wamefafanua kwa kina namna furaha na michezo hiyo ilivyozingatia mipaka ya kisharia katika zama za Mtume.

Katika matamshi ya hadith hizi, inabainika wazi kuwa ruhusa ya kuimba ilikuwa kwa wasichana wadogo, kwa kutumia dufu tu na si ala nyingine za muziki, wala isiwe tabia ya kawaida kama wasanii walivyoifanya kuwa sehemu ya maisha yao.

Ndiyo maana mama Aisha alisema: "Nao hawakuwa waimbaji." Hata katika michezo ya furaha siku ya Eid iliyofanyika karibu na nyumba ya Mtume, ambapo Wahabeshi walicheza kwa kutumia mikuki na ngao, mipaka ya dini ilizingatiwa kikamilifu.

Mama Aisha anasema: "Mtume alisimama nami nyuma yake nikitazama mchezo huo huku shavu langu likiwa juu ya shavu lake, naye akawaambia, 'Endeleeni enyi Banu Arfidah.'"

Hii inaonesha uzuri wa tabia ya Mtume alipowaruhusu wakeze kufurahia mambo ya halali huku akizingatia mipaka ya kisheria, bila kuchanganyika na wanaume. Michezo ya kutumia mikuki na ngao pia ilikuwa na lengo la kuimarisha miili na kuongeza ukakamavu.

## Ni siku ya ibada na furaha

Mafundisho haya yanaonesha kuwa furaha ya siku ya Eid ni sehemu ya dini. Mtume alikuwa mpole na mwenye kuwafurahisha wakeze, lakini furaha hiyo iliambatana na mipaka ya maadili na sharia za Kiislamu, si kufanya maasi au kuacha kumtii Allah.

Uislamu ni dini yenye wepesi na mizani ya uadilifu, hivyo Waislamu waepuke kudharau makosa madogo kwa hoja ya kusherehekea Eid. Matukio yaliyotokea mbele ya Mtume (rehema na amani zimshukie) yanatufundisha umuhimu wa kutendeana wema ndani ya familia, kuonesha upendo na kushiriki michezo ya halali.

Pia yanaonesha kuwa Uislamu ni dini yenye wasaa na haiwazuii watu mambo yenye faida, bali imeweka mipaka ya kuyaendesha kwa usahihi. Mtume alimkataza Abubakr kuwakemea wale wasichana na akawatia moyo kufanya mambo ya halali.

Hivyo, si vizuri kuwabana watu katika mambo ambayo Allah amewapa nafasi ya kuyafanya. Kilicho muhimu ni kutoa miongozo na kuwakumbusha kuwa mara nyingi mambo ya halali yanaweza kuwavuta watu kwenye haramu ikiwa hawatakuwa makini katika kuchunga mipaka ya Allah.

Sherehe za Eid ni kielelezo kuwa Uislamu unatambua mahitaji ya nafsi ya mwanadamu, ambayo wakati mwingine hupenda starehe na kupumzika. Kwa kuzingatia maumbile hayo ya kibinadamu, Uislamu umeweka nafasi ya kufurahi na kustarehe, lakini kwa sharti la kuheshimu mipaka ya dini. Hakuna uhuru usio na mipaka.

## Adabu na Sunna za kusherehekea Eid Takbira za Eid Kubadilisha njia na kupongezana

Ni vyema kuzingatia Sunna za Mtume (rehema na amani zimshukie) katika siku ya Eid, ikiwamo kuoga na kuvaa nguo nzuri. Ibn Qayyim (Allah amrehemu) amesema kuwa ni vizuri kuvaa nguo nzuri zaidi kwa ajili ya sala ya Eid na Ijumaa. Ama wanawake wanapotoka kwenda kusali Eid wanapaswa kutoka bila manukato na bila kujionesha.

Katika Eid ya Fitri ni Sunna kupiga takbira kuanzia usiku wa Eid mpaka sala ya Eid itakapoanza. Kwa Eid ya kuchinja (Udh'hiya), takbira huendelea mpaka siku za Tashriiq (tarehe 11, 12 na 13 Dhul–Hijjah). Vilevile, imesuniwa kutokula chochote kabla ya kusali Eid al–Adh'ha.






JUNAYNAT ALLY DAMA

# Tumia mwaka 1 – 5 kujengea msingi wa Imani, maadili kwa mtoto

Wataalamu wa malezi ya watoto wanasema umri wa miaka 1 hadi 5 ndiyo kipindi muhimu zaidi katika kujenga tabia, maadili na msingi wa imani kwa mtoto. Hiki ndiyo kipindi ambacho mtoto huanza kufyonza mazingira yanayomzunguka kwa haraka sana. Lakini wazazi wengi hupoteza fursa hiyo wakisubiri mtoto awe mkubwa ndipo waanze malezi ya kina ya kidini.

Tatizo ni kwamba mtoto anapofikia umri mkubwa zaidi, baadhi ya tabia tayari huwa zimejengeka. Ndiyo maana wataalamu wa tarbiyya wanasisitiza kuwa malezi ya kiimani hayapaswi kusubiri mpaka mtoto awe mkubwa kiasi cha kuelewa mihadhara mirefu. Yaanze mapema, kwa lugha rahisi, mazingira ya upendo na kwa vitendo vya kila siku.

Katika familia nyingi za Kiislamu, wazazi hujitahidi kuwafundisha watoto wao kuhifadhi dua mbalimbali. Hilo ni jambo jema. Lakini wakati mwingine watoto hukariri maneno ya Kiarabu bila kuelewa maana yake wala kujua wanamuomba nani.

Kumjua Allah si kuhifadhi maneno pekee. Ni kujenga hisia ya uwepo Wake katika maisha ya kila siku.

## Mbinu: Michezo na kurejeareja vitu

Watoto wa umri huu hawajifunzi zaidi kupitia mihadhara mirefu. Wao hujifunza kupitia kuona, kusikia, kucheza, kurudia vitu kila siku na kuhusisha maneno na mazingira yanayowazunguka.

Mzazi anapomfundisha mtoto kusema “Bismillah” kabla ya kula, anapaswa pia kumweleza kwa lugha rahisi kuwa chakula hicho ametupa Allah. Mtoto anaweza kugusa tunda, kuhisi ladha yake, kisha kuulizwa: “Ni nani aliyeumba kitu hiki kitamu?” Hapo mtoto anaanza kuunganisha neema anayoiona na Muumba wake.

Kadhalika, mtoto anapofundishwa dua ya kulala, ni muhimu pia kufahamu kuwa Allah ndiye anayemlinda hata gizani. Hapo dua haibaki kuwa maneno ya kukariri tu, bali inakuwa sehemu ya maisha yake.

Wataalamu wa malezi ya watoto wanaeleza kuwa watoto wa miaka 1 hadi 5 wana uwezo mdogo wa kuzingatia jambo kwa muda mrefu. Ndiyo maana si vizuri kuanza na dua ndefu au mafunzo magumu. Maneno mafupi kama “Alhamdulillah”, “SubhanAllah” au “Bismillah” huwa rahisi kwao kuyakumbuka na kuyafurahia.

Mtoto anapofanikiwa kutamka jambo dogo kwa usahihi, hupata hamasa ya kuendelea kujifunza zaidi. Ni sawa na mbegu ndogo inayoweza kuja kuwa mti mkubwa.

## Dua kama sehemu ya maisha

Njia nyingine muhimu ni kufanya dua ziwe sehemu ya kawaida ya maisha ya nyumbani badala ya kusubiri muda maalumu wa “darasa”. Mtoto akiamka asubuhi, wazazi waseme dua pamoja naye. Mvua ikinyesha, wamwite dirishani aangalie mvua huku wakisema dua ya mvua na kumweleza kuwa hiyo ni rehema ya Allah kutoka mbinguni.

Mnapoona ndege, maua au chakula kizuri, tumieni nafasi hiyo kusema “SubhanAllah” na kumkumbusha kuwa Allah ndiye Muumba wa vitu vyote vizuri anavyoviona.



Kwa mtoto mdogo, mambo yanayorudiwa kila siku huwa sehemu ya maisha yake ya kawaida. Bila kulazimishwa sana, anaanza kukua akiwa na mazoea ya kumkumbuka Allah katika mazingira tofauti.

Pia wataalamu wanashauri wazazi kutumia mbinu zinazoshirikisha hisia na vitendo. Mtoto hujifunza vizuri zaidi anapogusa, kuona, kusikia au kucheza. Ikiwa ni dua ya kula, zungumzeni kuhusu rangi, harufu na ladha ya chakula. Ikiwa ni dua ya mvua, muache asikie baridi ya dirisha au aangalie matone yanavyoshuka.

Mbinu hizi humsaidia mtoto kuelewa dini kwa namna ya maisha halisi badala ya kuhifadhi maneno yasiyo na uhusiano na mazingira yake.

## Malezi, somo la vitendo

Jambo muhimu zaidi ni kutambua kuwa tarbiyya si mashindano ya watoto wangapi wamekamilisha vitabu au kuhifadhi dua nyingi zaidi. Lengo kubwa ni kujenga moyo unaompenda Allah na unaohisi uwepo Wake katika maisha ya kila siku.

Mtoto anayekua katika mazingira hayo huwa na uwezekano mkubwa wa kuendelea kushikamana na dini hata anapokuwa mkubwa, kwa sababu imani yake haikujengwa juu ya kulazimishwa pekee, bali juu ya upendo, mazoea na uelewa.

Wakati mwingine wazazi huhisi ni vigumu kuwafundisha watoto wadogo mambo ya dini kwa njia ya furaha na urahisi. Lakini ukweli ni kwamba watoto wengi hupenda kujifunza wanapohusisha elimu hiyo na michezo, mazungumzo na mazingira yanayowazunguka.

Na hapo ndipo tarbiyya nzuri huanza — si kwa mihadhara mirefu, bali kwa maneno madogo, vitendo vya kila siku na moyo wa mzazi unaomwelekeza mtoto wake kwa Muumba wake.

MAKALA
SAIKOLOJIA

UKHTI FATIMA SS




# Tuwaelewe, tuwavumilia wenye majeraha ya kihisia

Wataalamu wa saikolojia wanasema si kila mtu anayekuwa mkali, mwenye hasira za mara kwa mara, anayejitenga na watu au anayewaumiza wanaompenda huwa ni mtu mbaya kwa asili. Wakati mwingine, tabia hizo huwa ni matokeo ya majeraha ya kihisia yaliyofichika ndani yake kwa muda mrefu.

Katika miaka ya karibuni, neno "trauma" limeanza kutumiwa sana katika mijadala ya afya ya akili. Kwa lugha rahisi, trauma ni athari za kisaikolojia zinazotokana na matukio magumu au yenye kuumiza ambayo mtu amewahi kupitia. Matukio hayo yanaweza kuwa kifo cha mpendwa, malezi ya ukatili, umasikini uliopitiliza, migogoro ya kifamilia, unyanyasaji, vita, ajali au hata kupuuzwa kihisia kwa muda mrefu.

## Anaweza kuumiza wanaompenda

Wataalamu wa afya ya akili wanaeleza kuwa majeraha ya kihisia yanaweza kubadilisha namna mtu anavyouona ulimwengu. Badala ya kuishi katika hali ya utulivu, akili huingia katika kile kinachoitwa "survival mode" — hali ya kujilinda muda wote.

Mtu mwenye trauma anaweza kuanza kuwa na hofu kubwa ya kuamini watu, kuwa mkali kupita kiasi, kujitenga na wengine au hata kusema uongo ili kujilinda dhidi ya maumivu ya kihisia anayoyaogopa.

Mara nyingi jamii huwaona watu wa aina hii kama wenye tabia mbaya tu bila kuelewa kile kilichowatokea nyuma ya pazia.

Wataalamu wa saikolojia wanaeleza kuwa akili ya binadamu ina mifumo ya kujilinda inapokutana na maumivu makubwa ya kihisia. Miongoni mwa mifumo hiyo ni kukataa ukweli, kukwepa mazingira yanayokumbusha maumivu, kulaumu wengine au kubadilisha simulizi za maisha ili mtu ajisikie salama zaidi kihisia.

Ndiyo maana wakati mwingine mtu aliyepitia majeraha makubwa anaweza kuwaumiza zaidi watu wanaompenda. Si lazima kwa sababu hana upendo, bali kwa sababu sehemu ya ndani yake bado inaishi katika hofu, maumivu au ukosefu wa usalama wa kihisia.

Pia wataalamu wanasema watu wengi wenye trauma hubeba hisia za aibu na kujilaumu. Wengine huamini kuwa wao ni "wameharibika", hawastahili kupendwa au watu wakiwajua vizuri watawaacha. Hisia hizi huathiri namna wanavyojenga mahusiano na kuwasiliana na wengine.

## Wana majeraha ya ndani, tuwavumilie

Katika jamii nyingi za Kiafrika, changamoto nyingine ni kwamba watu wengi wamelelewa kuvumilia maumivu badala ya kuyatibu. Mtoto anaambiwa "kuwa strong", "usiwe dhaifu" au "umezidi kufikiria sana" hata pale anapopitia maumivu ya kweli ya kihisia.

Matokeo yake, watu wengi hukua wakiwa wamebeba majeraha ya ndani kimya kimya huku wakionekana kawaida kwa nje.

Wataalamu wa afya ya akili wanaonya kuwa jambo ambalo limezoeleka katika jamii si lazima liwe zuri kiafya. Kuna watu wameishi maisha ya msongo, hofu au huzuni kwa muda mrefu kiasi kwamba wameanza kuona hali hiyo ni ya kawaida.

Lakini kuzoea maumivu si sawa na kupona.

Kwa mujibu wa wataalamu wa saikolojia, kupona kihisia hakumaanishi mtu anakuwa binadamu mpya kabisa. Mara nyingi huanza kwa kubadilika kwa namna anavyoyaona maisha na alivyojiona mwenyewe. Mtu anaanza kuelewa kuwa kile alichopitia si lazima kiendelee kutawala maisha yake yote.

Safari ya kupona inaweza kujumuisha kuzungumza na wataalamu wa afya ya akili, kupata watu salama wa kuwasikiliza, kujifunza kuelewa hisia zake na kuanza kujijengea mazingira yenye utulivu wa kihisia.

Aidha, wataalamu wanasisitiza umuhimu wa jamii kuwa na huruma zaidi katika namna inavyowachukulia watu wenye changamoto za kihisia. Si kila anayekuwa mkimya ana kiburi. Si kila mwenye hasira nyingi ni mwenye roho mbaya. Wengine wanapambana na maumivu ambayo hayionekani kwa macho.